# Nipashe

Jumamosi Januari 2, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580448

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




**Chelsea yatangaza kupata faida**

UKURASA 20

**Mbaroni** tuhuma kumuua baba yake kisha kumfukia

UKURASA 2



**Kalemani** atangaza fursa za ajira kwa vibarua TANESCO

UKURASA 4

# TRA yaweka rekodi ukusanyaji mapato

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### AUAWA NA POLISI TUHUMA UJAMBAZI

JESHI la Polisi mkoani Kigoma, limemuua mtu mmoja anayedai-

UKURASA WA 5

### WAKURUGENZI WABAINIKA KUTELEKEZA IDARA ZA ARDHI

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendelea ya Makazi, Dk. Angeline...



Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Doto James, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kufanikiwa kukusanya kiasi cha Sh. trilioni 2.088 kwa kipindi cha mwezi Desemba 2020. (Kushoto) Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato, Dk. Edwin Mhede na Naibu Kamishna, Msafiri Mbibo. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Mgogoro ujenzi wa barabara wamwibua waziri

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store




## Rais Mwinyi ateua mwanamke wa kwanza Katibu Mkuu Kiongozi

UKURASA 10

**MICHEZO** **YANGA: MSIMU HUU HATUTAPOA** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Mbaroni akidaiwa kumuua baba yake

**Na Samson Chacha,** TARIME

MKAZI wa Kijiji cha Pemba, Tarafa ya Inchugu wilayani Tarime mkoani Mara, Burure Mniko, anashikiliwa na Jeshi la Polisi Kituo cha Sirari, akituhumiwa kumuua baba yake mdogo aitwaye Chiranye Mniko.

Inadaiwa mtuhumiwa huyo alimuua baba yake mdogo huyo baada ya kutokea ugomvi usiku wakitokea kwenye ulevi na kisha kumzika jirani na nyumba yake.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Pemba, Christopher Wantora, alisema tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia Jumatano Desemba 30, nyumbani kwao walipokuwa wakiishi baada ya kutokea ugomvi kati yao.

Alisema kuwa ilipofika asubuhi, baadhi ya majirani waliokuwa wamesikia kelele na ugomvi kati ya Burure na Chiranye, walitaka kujua kilichotokea na ndipo walipoona kaburi lililochimbwa na kufukiwa na kutia shaka.

Kiongozi huyo wa kijiji alisimulia kuwa, huku kukiwa na kaburi hilo, hapakuwa na mtu yeyote kwenye mji huo, ndipo walipoanza kuwasaka ndugu hao wawili waliokuwa wakipigana usiku na wakapata fununu kuwa Burure ameonekana Kijiji cha Ngerengere, Kata ya Regicheri.

Alisema kuwa baada ya kupata taarifa ya mtuhumiwa huyo, walikodi pikipiki (bodaboda) na kutoa taarifa Kituo cha Polisi Sirari na kufanikiwa kumkamata Burure na kumrejesha hadi nyumbani kwao na kisha kufukua kaburi alilokuwa amemzika ndugu yake huyo.

Wantora alisema kuwa baada ya kufukua, waliukuta mwili wa ndugu yake ambao ulichukuliwa na polisi kwa ajili ya uchunguzi zaidi.

Kamanda wa Polisi Tarime/Rorya, William Mkonda, alithibitisha kutokea kwa mauaji hayo, akisema: "Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi kuhusiana na matukio hayo na tunawaasa wananchi kutojichukulia sheria mkononi kwa kuwaua wenzao."

# TRA yaweka rekodi mpya ukusanyaji mapato

**Na Enock Charles**

MAMLAKA ya Mapato (TRA), imekusanya Sh. trilioni 2.088 Desemba 2020, ikivuka lengo lake la kukusanya Sh. trilioni 2.072, kikiwa ni kiwango kikubwa zaidi kukusanywa na taasisi hiyo kwa mwezi.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Kamishna Mkuu wa TRA, Dk. Edwin Mhede, alisema wamefanikiwa kukusanya kiwango hicho cha fedha kutokana na wafanyakazi kufanya kazi kwa kujituma na weledi pamoja na kupata ushirikiano mzuri kutoka kwa walipakodi.

"Mamlaka ya mapato isingekusanya endapo walipakodi wasingekuwapo. Tunawapongeza kwa kutimiza wajibu wenu wa kisheria ambao kwa kweli umeleta kodi hizo za hiari, ndiyo umetufikisha hapa tulipofika," alisifu.

Dk. Mhede alibainisha makusanyo yao kwa miezi sita ya awali ya mwaka huu wa fedha, akifanya kuwa Julai walikusanya Sh. trilioni 1.2, Agosti Sh. trilioni 1.3, Septemba Sh. trilioni 1.7, Oktoba Sh. trilioni 1.3, Novemba Sh. trilioni 1.3.

Aliupongeza Mkoa wa Dodoma kwa kukusanya Sh. bilioni 17, ikiwa ni zaidi ya lengo uliojiwekea.

Kamishna Mhede alisema makusanyo hayo ya miezi sita ni ya wastani wa Sh. trilioni 1.6 kwa mwezi kulinganishwa na wastani wa Sh. trilioni 1.5 kwa mwaka 2019/20.

"Katika mikoa mikubwa, kuna mkoa mmoja umefanya vizuri na umevuka lengo hadi sasa na huu ni Mkoa wa Dodoma.

"Pamoja na changamoto zilizopo Dodoma za matumizi hafifu ya EFD, wamefika asilimia 127 kwa kukusanya zaidi ya Sh. bilioni 17. Hawa tayari siyo wadogo tena.

"Kwa msingi huo, sasa tunapeleka huduma zaidi Dodoma," Kamishna Mhede alisema.

Akizungumza katika mkutano huo na waandishi wa habari, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Doto James, licha ya kuipongeza TRA kwa kukusanya kiwango hicho cha fedha, alisema bado lipo tatizo kubwa la baadhi ya wafanyabiashara na wananchi kutokutumia risiti za EFD.

Alisema dosari hiyo inasababisha upotevu mkubwa wa mapato ya nchi, hivyo kuwaonya wale ambao hawataki kutoa au kuomba risiti wanapouza au kununua bidhaa kuwa serikali itaendelea kuwachukulia hatua za kisheria kila wanapobainika.

James alisema lengo la mkazo huo ni kuiwezesha serikali kukusanya kiwango kikubwa zaidi cha kodi ambayo inategemewa katika kutoa huduma kwa wananchi.

"Hakuna serikali halali popote duniani ambayo haikusanyi kodi, hivyo tutaendelea kubana mianya yote ya ukwepaji kodi.

"Kuna watu wanadhani kukwepa kodi ndiyo eti ni mazingira mazuri ya kufanya biashara. Hiyo siyo sahihi, serikali itaweka mazingira mazuri, lakini pia tutadhibiti ukwepaji kodi," alisema.

Katibu Mkuu huyo alisema wapo wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu, ambao wamekuwa wakipeleka nyaraka za kughushi katika mamlaka za kiserikali ili kupewa marejesho ya kodi kwa madai wameuza bidhaa nje ya nchi.

Alisema kuwa uchunguzi unapofanyika, wamekuwa wakigundulika kuwa hakuna biashara yoyote ama iliyonunuliwa au kuuzwa nje ya nchi, akionya vikali kuhusu tabia hiyo.



Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa (kulia), akiwa ameambatana na Mkuu wa Wilaya ya Karagwe, Godfrey Mheruka na wafanyabiashara wa mji wa Kayanga wakikagua majengo ya maduka yaliyoungua kwa moto uliotokea Desemba 26, 2020 katika mji wa Kayanga, Karagwe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mgogoro mkataba ujenzi barabara wamwibua waziri

**Na Mwandishi Wetu**

MGOGORO wa ujenzi wa barabara ya Mikumi- Ifakara, sehemu ya Kidatu- Ifakara umemwibua Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Dk. Leonard Chamuriho na kutaka umalizwe mara moja.

Kutokana na mgogoro huo, waziri ameagiza Baraza la Ujenzi la Taifa (NCC) kukutana na Wizara ya Fedha na Mipango, Mkandarasi na Mhandisi Mshauri ili kuutatua na hatimaye kazi hiyo kuendelea.

Akizungumza jana baada ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa barabara hiyo, Dk. Chamuriho alisema uwapo wa mgogoro huo unachangia ucheleweshaji wa ukamilishaji wa mradi, hivyo kuwacheleweshea wananchi maendeleo.

"Kutoelewana kati ya wadau wote wanaojenga barabara ni tatizo ambalo linasababisha mradi kutojengwa kwa kasi. Tunahitaji changamoto hizo mzikamilishwe na mradi ukamilike kwa wakati," alisema.

Pia aliuagiza Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kuhakikisha changamoto zote zinazoainishwa baada ya kikao cha wadau zinatekelezwa kwa kuzingatia makubaliano.

Meneja wa TANROAD Mkoa wa Morogoro, Mhandisi Nkolante Ntije, alimhakikishia Waziri Chamuriho kuwa watatekeleza maelekezo na kuwasilisha taarifa wizarani ndani ya muda mfupi.

Katika hatua nyingine, Waziri Chamuriho alikagua ujenzi wa barabara ya Dumila -Kilosa- Mikumi, sehemu ya Rudewa - Kilosa (km 24) na kuridhishwa na maendeleo ya ujenzi wake na kuwataka makandarasi wazawa Umoja - Kilosa JV kuongeza kasi ili mradi ukamilike kwa wakati.

Msimamizi wa Mradi huo, Mhandisi Robert Mwita, alisema pamoja na uwapo wa mvua, mradi unaendelea kutekelezwa na unatarajiwa kukamilika mapema Agosti, mwaka huu.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akijumuika na wanamichezo wa mazoezi ya viungo, katika Tamasha la Mazoezi ya Viungo Kitaifa Zanzibar, lililofanyika viwanja vya Mapinduzi Square Michezani na kumalizikia Uwanja wa Amaan, jana. (Kulia kwake) Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad. **PICHA: IKULU**

# Mwinyi aahidi kutatua kero wafanyakazi sekta ya afya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, ameahidi kuzitafutia ufumbuzi kero zinazowakabili wafanyakazi wa sekta ya afya.

Akizungumza katika kikao chake na wafanyakazi hao katika Ukumbi wa Shekhe Idrissa Abdulwakili Kikwajuni juzi, Dk. Mwinyi alisema anatambua mfumo wa afya una utaratibu wake ili ukamilike ikiwamo miundombinu.

“Tunatambua miundombinu ya afya haijakamilika, hatuwezi kujenga hospitali mpya kwa siku moja, lakini mipango ya kujenga hospitali mpya ya rufani ipo,” alisema.

Alisema mfumo mwingine unagusa wafanyakazi, akifafanua kuwa bila wafanyakazi, huduma bora zitakosekana, hivyo atahakikisha anaongeza wataalamu watakaofanya kazi.

Dk. Mwinyi pia alizungumzia upatikanaji wa vifaa tiba na dawa, akibainisha kuwapo kwa kasoro kubwa kutokana na matumizi mabaya ya fedha na tatizo katika utoaji wa dawa.

“Huu ni wakati wa kuwatumbua watu wasiowajibika kwa sababu wananchi wanaumia, hebu tujifunze kwa wenzetu Tanzania Bara jinsi wanavyosambaza dawa,” aliagiza.

Alisema eneo lingine ni fedha, akifafanua kuwa bila ya fedha, uendeshaji wa hospitali hautafanyika, hivyo mbali na bajeti ya Wizara ya Afya, kuna mipango mingine mbadala ya kupata fedha.

Dk. Mwinyi alisema kuna tatizo la uongozi katika sekta ya afya, akieleza kuwa wakubwa wamezoea kukaa ofisini badala ya kwenda katika hospitali kujua matatizo yaliyopo.

Alisema lazima kutoa huduma bora na yule ambaye atashindwa kutoa huduma bora, atamwondoa.

“Kuna haki na wajibu, tunapowajibika vizuri, haki itapatikana. Sisi wafanyakazi wa afya tuna jukumu la kutoa huduma bora za afya,” alisema.

Aliongeza kuwa lugha nzuri ni nusu ya tiba, hivyo watoa huduma za afya wajitahidi kuwa na lugha nzuri kwa wananchi wanaofuata huduma za afya.

Alisema huwezi kufanya matibabu bila kujua magonjwa yaliyopo, akiwataka wafanyakazi wa sekta hiyo, hasa viongozi, kuwajibika ipasavyo.

Kiongozi huyo wa juu serikalini, aliwapongeza watendaji wa afya wanaowajibika licha ya mazingira magumu ya kazi yanayowakabili.

Alisema wakati umefika wa kuwa na bima za afya na kuwataka viongozi kukutana na wafanyakazi mara kwa mara ili kutatua vikwazo vilivyopo.

Vilevile, Dk. Mwinyi aliwataka viongozi kuwa wabunifu katika kutatua matatizo yanayojitokeza.

Akizungumzia kuhusu ugatuzi, alisema ni lazima kufanya tathmini ili kuona kama kuna haja ya kuendelea na ugatuzi au la.

**VILIO VYA WAUGUZI**

Katika kikao hicho, baadhi ya wafanyakazi wa Wizara ya Afya Zanzibar, wakiwamo wauguzi, wakunga na madaktari, waangusha kilio mbele ya Dk. Mwinyi kutokana na mazingira magumu ya kazi katika kutoa huduma za afya.

Wafanyakazi hao walisema kuwa wanafanya kazi katika mazingira magumu ili kuokoa maisha ya wananchi hasa katika huduma za mama na mtoto.

Umurukhurthum Hamad, Mkuu wa Idara ya Huduma za Mama na Mtoto, alisema ili vifo vya mama na mtoto vipungue, ni lazima kuwekeza katika vifaa tiba na rasilimali watu, hasa madaktari.

Alisema kuna vikwazo vingi katika huduma za afya ya mama na mtoto ikiwamo upungufu wa madaktari, wauguzi na wakunga.

Hamad alisema Hospitali ya Muembeladu ambayo hutoa huduma za mama wajawazito pekee, iko katika hali mbaya na huduma zinatolewa siyo za kuridhisha kwa sababu hakuna madaktari bingwa.

Alisema kitaalamu muuguzi mmoja anatakiwa kuhudumia mama wajawazito wawili, lakini kwa sasa muuguzi mmoja anahudumia wagonjwa 10, jambo ambalo halileti ufanisi mzuri wa kazi.

Alisema kuwa wanafanya kazi katika mazingira magumu bila kupewa posho ya muda wa ziada wa kufanya kazi.

“Licha ya mazingira magumu ya kufanya kazi, tunapambana katika kuokoa vifo vya mama na mtoto na kwa mwaka 2019, kulikuwa na vifo vya mama na mtoto 309 na kwa mwaka huu (2020) ni 141,” alisema.

Aliongeza kuwa wanahitaji vifaa tiba ili kunusuru vifo vya mama na watoto kwa kuwa vifaa vilivyopo havitoshi kudhibiti vifo vya mama na mtoto.

Sabra Amour kutoka Kitengo cha Maabara Hospitali ya Mnazimmoja, alisema mashine nyingi za uchunguzi wa maradhi hazifanyi kazi na hakuna wataalamu wa kuzifanyia matengenezo.

Alisema kikwazo kingine ni uchakavu wa jengo la maabara na uhaba wa wafanyakazi katika maabara.

Faudhia Abdullah kutoka Hospitali ya Makunduchi, alisema kuwa hospitali hiyo haiko salama na wakati mwingine wanaibiwa kwa sababu haina uzio.

“Afya bure imekuwa na changamoto kubwa, tunakosa usingizi, wauguzi tunafanya kazi katika mazingira magumu sana, ninaomba utusaidie Mheshimiwa Rais,” alisema.

Aliongeza kuwa kuna urasimu mkubwa katika Wizara ya Afya, hasa wanapoomba nafasi za masomo.

## Auawa na polisi tuhuma ujambazi

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

JESHI la Polisi mkoani Kigoma, limemuua mtu mmoja anayedaiwa kuwa jambazi, huku wenzake watatu wakidaiwa kukimbia wakati walipokuwa wakitaka kutekeleza uhalifu juzi majira ya saa tano na nusu usiku maeneo ya Shayo, Kata ya Mrusi wilayani Kasulu.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kigoma, James Manyama, alisema jeshi hilo likiwa katika doria za kuimarisha ulinzi na usalama wakati wa mkesha wa Mwaka Mpya, lilipokea taarifa za watu wanaopanga kutekeleza tukio la uhalifu.

Kamanda Manyama alidai kuwa askari polisi walifika mapema eneo la tukio na baada ya watu hao kuona askari, walianza kurushiana risasi na askari zilizosababisha kijana mmoja anayekadiriwa kuwa na umri wa kati ya miaka 30 hadi 35 kujeruhiwa na kupoteza maisha akiwa anapelekwa hospitali kwa ajili ya matibabu.

Alisema kuwa katika tukio hilo, silaha aina ya AK 47 ambayo namba zake zimefutwa, iliokotwa na askari kwenye eneo la tukio pamoja na magazine moja yenye risasi 13, mapanga mawili na nondo iliyokatwa.

Kamanda Manyama alitoa onyo kwa wananchi wanaojihusisha na vitendo vya uhalifu mkoani Kigoma, akiwataka kuacha mara moja kwa kuwa jeshi hilo limejipanga kukabiliana na uhalifu huo.

“Uhalifu kwa sasa katika Mkoa wa Kigoma siyo dili, ukija na ‘kasilaha kako’, tunakunyang’anya mara moja,” Kamanda Manyama alitamba.

Matukio ya ujambazi yamepungua nchi tangu kutolewa kwa agizo kwa askari polisi kunyang’anya silaha majambazi, amri iliyotolewa mwanzoni na uongozi wa serikali ya awamu ya tano.

# Askofu ataka serikali kuheshimu wataalamu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

ASKOFU Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Dodoma, Beatus Kinyaiya, amewataka viongozi wa serikali kutumia wataalamu katika utekelezaji wa majukumu yao, badala ya kulaumu pale yanapoharibika.

Aidha, ameipongeza serikali kutokana na maendeleo iliyofanya katika kipindi chote cha mwaka 2020.

Askofu Kinyaiya, aliyasema hayo katika ibada ya mkesha wa Mwaka Mpya iliofanyika Kanisa Kuu la Mtakatifu Paulo wa Msalaba wakati akitoa mahubiri mbele ya waumini waliohudhuria ibada hiyo.

"Viongozi wa serikali uwe waziri, mbunge na viongozi wengine hata kama mmepewa madaraka, watumieni wataalamu kutekeleza maendeleo katika maeneo mbalimbali mnayosimamia na si kuagiza bila kutumia wataalamu. Matokeo yake mnakuja kuleta malumbano pale kazi inapoharibika," alisema.

"Unaweza ukawa waziri, lakini huna ujuzi na mradi unaokwenda kutekelezwa. Ni vema ukatumia nafasi yako kutafuta wataalamu ili wasaidie kutekeleza majukumu," aliongeza.

Alisema maendeleo ya nchi ni ya kila mmoja, hivyo hakuna sababu ya waziri kusimamia kazi kwa kutoa maagizo bila kutumia wataalamu ambao wanaweza kusaidia utekelezaji wa mradi ukaomalizika bila ya kuleta malumbano.

Askofu Kinyaiya aliwataka Watanzania kumshukuru Mungu kutokana na taifa kuwa na amani tofauti na nchi zingine ambazo machafuko imekuwa kitu cha kawaida kwao.

Alisema Watanzania wanapaswa kumshukuru Mungu kwa amani walio nayo ambayo haipaswi kuichezea badala yake wailinde kwa kufanya matendo mema.

"Hivi karibuni tumetoka kwenye uchaguzi na umemalizika kwa amani kinachotakiwa ni kuisaidia serikali kulinda amani iliyopo kwa kutenda matendo ya kumpendeza Mungu, hivyo kila mmoja kwa nafasi yake anapaswa kuomba na kushukuru," alisema.



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, akikagua maendeleo ya ujenzi wa Ofisi ya Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) Kanda ya Mashariki iliyopo Kibaha, Mkoa wa Pwani, wakati wa ziara ya kukagua utendaji kazi wa sekta ya ardhi na miradi inayotekelezwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC). Kulia ni Meneja wa Huduma za Jamii na Uhusiano wa Shirika la Nyumba la Taifa, Muungano Saguya. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

# Kalemani atangaza neema vibarua TANESCO

**Na Dorina Makaya,** SHINYANGA

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, ametangaza neema kwa vibarua wa muda mrefu Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) nchi nzima, kutaka waombewe ajira.

Waziri Kalemani alitoa agizo hilo juzi alipokuwa akizungumza na watumishi wa TANESCO wa Mkoa wa Shinyanga, katika kikao kazi cha kufahamiana, kusikiliza kero na kutoa maelekezo ya kazi.

Lengo la kikao hicho lilikuwa kuweka mkakati wa kuliwezesha shirika kufanya kazi kama timu moja kwa kasi kwa ubunifu na kwa usahihi, ili kufikisha huduma ya umeme kote nchini na kuongeza mapato ya serikali kutokana na sekta ya nishati.

Akizungumza baada ya kusikiliza kero za watumishi, Waziri Kalemani aliweka bayana kuwa watumishi hao wanaoajiriwa kwa vipindi vifupi ndio wanaokutana na wateja moja kwa moja na kujenga taswira ya TANESCO.

Alisema kufanya kazi kama kibarua kwa miaka mingi bila kuajiriwa kwa watumishi hao, kunapunguza na pengine kuondoa ari ya kufanya kazi, kuleta mianya ya rushwa na hata kutengeneza vishoka.

Dk. Kalemani alisema anaamini kuajiriwa kwa watumishi hao kutawajengea kufanya kazi kwa uaminifu na kwa kujituma kwa kuwa watahitaji kutunza ajira zao na kuonya kuwa mtumishi yeyote atakayebainika anaomba rushwa kutoka kwa wateja na kutumia lugha zisizofaa, ataondolewa mara moja na hatua za kinidhamu kuchukuliwa dhidi yake.

Kuhusu umuhimu wa kikao kazi hicho, Waziri Kalemani alisema ili kuwezesha utekelezaji mzuri wa kazi, iko haja ya kuonana na watumishi, kufahamiana, kujionea mazingira halisi ya kazi, kusikiliza kero zao na kuzitolea ufumbuzi na kisha kutoa mwelekeo na maelekezo ya kazi kufikia malengo yaliyowekwa.

"Unaweza kuwa unaagiza, nataka kazi hii ifanyike leo na kukamilika leo hii hii kumbe unayempa maelekezo hayo ni mlemavu (mwenye ulemavu) na hana uwezo wa kwenda kwa kasi hiyo. Ukaagiza afukuzwe kwa kushindwa kutekeleza kazi husika, lakini kumbe uliyemwagiza ni mlemavu, hivyo ni muhimu kufahamiana," alisema.

Waziri pia aliagiza TANESCO kuwanunulia pikipiki watumishi walio katika vitengo vya upimaji kwa ajili ya kufikisha umeme kwa wateja ili kuwezesha utendaji kazi kwa haraka. Aliawelekeza watumishi hao kuzitumia pikipiki hizo kwa shughuli za kikazi.

"Msije mkazigeuza pikipiki hizo kuwa bodaboda. Tena mziandike SU. Nataka mfanye kazi kwa kasi, kwa ubunifu, na kwa usahihi," alisema na kuongeza kuwa: "Nataka kila ofisi ya TANESCO ninayokwenda nione kuna ongezeko la mapato, nione kuna ongezeko la wateja sugu kulipa madeni wanayodaiwa na TANESCO."

Katika hatua nyingine, Waziri Kalemani aliiagiza TANESCO na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kuhakikisha vijiji vyote nchini vimeunganishwa na umeme ifikapo Septemba, 2022.

# Njombe yatangaza vita mikopo umiza

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

HALMASHAURI ya Mji wa Njombe imejipanga kupambana na mashirika ya kilimo yanayotoa mikopo kandamizi ya pembejeo kwa wakulima, kwa kutoa misaada kwa kivuli cha mashirika yasiyo ya kiserikali wakati ni kampuni za kibiashara.

Hatua hiyo inatokana na malalamiko kutoka kwa wakulima kuingia kwenye migogoro na mashirika hayo baada ya kushindwa kurejesha mikopo kwa sababu ya ulaghai unaofanywa na baadhi yao.

Akizungumza katika kikao cha mrejesho wa mradi wa kilimo kutoka Shirika la Highlands Hope Umbrella (HHU) unaotekelezwa katika Tarafa ya Igominyi, Ofisa Kilimo Kata ya Kifanya kwa niaba ya wakulima, Suzana Kiwele, alisema wamekuwa wakipokea malalamiko kutoka kwa wakulima wakirubuniwa pembejeo kwa kukopeshwa kwa bei nafuu, ili hali wakati wa mavuno wamekuwa wakilipa zaidi ya makubaliano.

"Mkulima anapenda sana afanikiwe kwa hiyo akiona shirika linatoa labda mbolea hawezi kuacha. Sasa tunapata malalamiko kwa kuwa awali mashirika yanakuja kwa lugha tamu ila mwisho wa siku baada ya mavuno riba yake inakuwa kubwa tofauti na walichokipata," alisema Kiwele.

"Ili kuondoa malalamiko ya mara kwa mara, niwaombe wakulima wajenge msingi wa kujitegemea kuliko kuendesha kilimo kwa mikopo kwa kila kitu na wakopeshaji wengine wako kibiashara zaidi," alisema Onesmo Kamonga, Ofisa Ugani kata ya Iwungilo.

Naye Mkurugenzi wa HHU, Bethseba Liduke, alisema kwa sasa wameingia katika kilimo ili kuongeza nguvu ya mabadiliko ya kilimo bora ufanisi na chenye tija mkoani Njombe, huku akiwashauri wakulima kuwa makini na mashirika yanayofika kwenye maeneo yao pamoja na serikali kuendelea kupambana na mashirika umiza.

"Safari hii tumeingia kwenye kilimo kwa sababu kwa Njombe ni uti wa mgongo, lakini wakulima wamekuwa na kilimo cha mazoea. Tunachohitaji watu walime kilimo bora chenye ufanisi na kitakacholeta matokeo chanya kwa mkulima," alisema.

Ofisa Mazao Halmashauri Ya Mji Njombe, Nolasco Kilumile, alisema mashirika mengi yanakuja kwa mgongo wa NGO, lakini yanafanya biashara, hivyo akawataka wakulima kukopa kwa hiari yao na kujenga utamaduni wa kuwa na mitaji yao wenyewe.

**HABARI KITAIFA**

## DC ahimiza ujenzi wa madarasa

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

SERIKALI imewataka viongozi wa kata na vijiji kuhakikisha wanajenga shule katika maeneo yao, ili wanafunzi wanaolazimika kutembea umbali mrefu kutafuta elimu, wawe wanaipata karibu na makazi yao.

Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga, Dk. Khalfan Haule, alitoa rai hiyo alipozungumza na waandishi wa habari waliofika ofisini kwake kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa mpango mkakati wa kutokomeza mimba za utotoni ulioanzishwa na Mkoa wa Rukwa.

Mpango wa kukabiliana na mimba na ndoa za utotoni unatekelezwa na Shirika lisilo la kiserikali la YES- Tanzania (Youth Education Through Sports) kwa ufadhili wa shirika lisilo la kiserikali la Plan International mkoani Rukwa.

Alisema miongoni mwa sababu zinazochangia wanafunzi wengi kupata ujauzito, ni kutembea umbali mrefu kufuata masomo, akibainisha kuwa wilaya hiyo ina kata 10 ambazo hazina shule za sekondari.

Alisema kuwa iwapo kata hizo zitajenga shule za sekondari na kila kijiji kikipata shule ya msingi, itakuwa ni ngumu kwa wanaume wenye tabia ya kuwashawishi wanafunzi kujiingiza kwenye vitendo vya mapenzi, kufanikiwa katika hilo kwa kuwa wazazi wao na jamii itawalinda.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga, Nyangi Msemakweli, alisema kuwa pamoja na utekelezaji wa agizo hilo, halmashauri hiyo ina mpango wa kuhakikisha kila shule ya msingi na sekondari inaanza kutoa chakula kwa wanafunzi mwaka huu.

Kaimu Mganga Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga, Nicodemus Masosota, alisema kuwa tangu kuanzishwa kwa mpango wa kupambana na mimba za utotoni mwaka 2018 ambao utamalizika mwaka 2022, tayari matokeo chanya yamekwishaonekana kwa kuwa mwaka 2019 ziliripotiwa mimba 39 na mwaka jana ziliripotiwa mimba 12 wilayani humo.



Baadhi ya wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu wa Handali iliyopo Chamwino mkoani Dodoma, wakishiriki mkutano na Naibu Waziri wa Madini, Prof. Shukrani Manya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakurugenzi wabainika kutelekeza idara za ardhi

**Na Munir Shemweta,** KIBAHA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendelea ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amewajia juu baadhi ya wakurugenzi wa halmashauri kwa kushindwa kuzihudumia idara za ardhi katika halmashauri zao na kuzifanya idara hizo kufanya kazi katika mazingira magumu.

Dk. Mabula alibainisha dosari hiyo alipozungumza na watendaji wa sekta ya ardhi, uongozi wa mkoa wa Pwani na wakurugenzi wa halmashauri za mkoa huo, juzi, akiwa katika ziara ya kukagua utendaji kazi wa sekta ya ardhi na kukagua miradi inayotekelezwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) mkoani humo.

Alisema kuna baadhi ya wakurugenzi wa halmashauri wamekuwa wakorofi na kuziona idara za ardhi kama siyo sehemu ya idara zao na kuziacha bila kuzihudumia.

Alisema kuwa baada ya kutoka waraka uliohamisha maofisa ardhi kurudi Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kuna baadhi ya wakurugenzi wa halmashauri waliamua kujivua kuzihudumia idara hizo kwa kisingizio kuwa idara hizo sasa haziko chini yao na zimerejeshwa wizarani.

Dk. Mabula alisema waraka uliotolewa na kusambazwa kwa makatibu tawala wa mikoa, uliweka wazi kuwa wajibu wa Wizara ya Ardhi kwa watumishi wa sekta hiyo, utakuwa kwenye masuala ya sera, ajira na nidhamu, lakini usimamizi utaendelea kubaki kwa wakurugenzi wa halmashauri.

Kwa mujibu wa Dk. Mabula, majukumu ya kupanga miji ni ya halmashauri za miji, manispaa na majiji, hivyo wakurugenzi wa halmashauri bado wana wajibu wa kuzihudumia idara hizo ili zipange miji vizuri pamoja na kutoa huduma zinazohusiana na masuala ya ardhi.

"Hawa ni watumishi wenu kama walivyo wale wa idara nyingine za afya, elimu na zinginezo, hivyo mnapaswa kuwahudumia vizuri ikiwamo kuwapatia vitendea kazi, ili waweze kufanya kazi vizuri," aliagiza.

Dk. Mabula aliwataka wakurugenzi wa halmashauri kubadilika na kuanza kuzihudumia idara za ardhi vizuri kwa kuzipangia idara hizo bajeti ya kutosha pamoja vitendea kazi kama magari na vifaa vya kupimia ili zitekeleze majukumu yake kwa ufanisi.

Akigeukia suala la ukusanyaji maduhuli ya serikali kupitia kodi ya pango la ardhi, akiwataka wakurugenzi wa halmashauri zote nchini kuziwezesha idara za ardhi ili zifuatilie madeni ya wadaiwa sugu wa kodi ya ardhi katika maeneo mbalimbali.

Kwa mujibu wa Dk. Mabula, Mkoa wa Pwani pekee unadai Sh. bilioni 32.763 za kodi ya pango la ardhi kutoka kwa wadaiwa mbalimbali na kusisitiza kuwa kama idara za ardhi zitawezeshwa vizuri, zinaweza kukusanya mapato mengi yatakayosaidia utekelezaji miradi mbalimbali kama vile ya afya, elimu na miundombinu kulinganisha na idara zingine.

Mkuu wa Kitengo cha Kodi Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Denis Masamia, alisema pamoja na mikakati iliyowekwa na wizara yake katika kukusanya kodi, bado kuna kazi kubwa ya kufanya katika suala hilo.

Alibainisha kuwa hadi kufikia Desemba 31 mwaka jana, ni Sh. bilioni 61 zilizokuwa zimekusanywa na kutaka juhudi za makusanyo kuongezwa katika kila halmashauri.

Malengo ya wizara katika mwaka wa fedha 2020/21 ni kukusanya Sh. bilioni 200, hivyo makusanyo yaliyopatikana katika miezi sita ya mwanzo wa mwaka wa bajeti, hayajafika hata nusu ya malengo.

Katika hatua nyingine, Dk. Mabula alitembelea na kukagua mradi wa ujenzi wa Ofisi ya Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) Kanda ya Mashariki ulioko wilayani Kibaha mkoani Pwani, ukitekelezwa na NHC.

# 'Viongozi vyama vya watu wenye ulemavu washirikiane na serikali'

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Watu Wenye Ulemavu), Ummy Nderiananga, amewataka viongozi wa vyama vya watu wenye ulemavu, kuhakikisha wanashirikiana na serikali, ili kuimarisha ustawi na kuchochea gurudumu la maendeleo kwa kundi hilo.

Alitoa rai hiyo jana alipokutana na viongozi wa vyama vya watu wenye ulemavu jijini Dar es Salaam kwa lengo la kujadiliana na kushauriana namna bora ya kuhudumia watu wenye ulemavu na kutatua kero zinazowakabili nchini.

Ummy alisema serikali inawajali na kuwathamini watu wenye ulemavu na kwa kulitambua hilo, imekuwa ikishirikiana na asasi za watu wenye ulemavu kutetea maslahi ya kundi hilo katika jamii inayowazunguka.

"Mkiwa kama viongozi wa vyama vya watu wenye ulemavu, mtambue mna jukumu na ni wajibu wenu kushughulikia masuala mbalimbali ya wenye ulemavu kwa kushirikiana na serikali, ili kufanikisha malengo mliyonayo.

"Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dk. John Magufuli, imekuwa ikitatua matatizo ya wananchi papo kwa papo na ndivyo tulivyoelekezwa sisi watendaji wake kutatua kero za wananchi na ndiyo maana nipo hapa kusikiliza kero zenu na kuzitafutia ufumbuzi," alisema.

Ummy alisema viongozi wa vyama vya watu wenye ulemavu wanatakiwa kutambua majukumu yao na kuyatekeleza kwa weledi na ufanisi ili kufanikisha masuala mbalimbali yanayolikabili kundi hilo

Aliongeza kuwa watu wenye ulemavu wana uwezo wa kufanya miradi mikubwa ambayo itawawezesha kujikwamua kiuchumi na kuajiri wenzao wengine wenye ulemavu, hivyo akawataka viongozi wa vyama hivyo nchini, kuanzisha miradi mikubwa.

Naibu waziri huyo pia aliwataka maofisa ustawi wa jamii kuongeza juhudi na kasi katika kuhamasisha watu wenye ulemavu wananufaika na fursa ya mikopo inayotolewa na halmashauri ya mbili ya mapato ili wajikwamue kiuchumi.

Alitaka uwapo utaratibu mzuri na ambao utakuwa rafiki kwa watu wenye ulemavu kupata mikopo hiyo inayotolewa na halmashauri pasipokuwa na vikwazo vyovyote.

"Watu wenye ulemavu wanapokuja kuomba mikopo hiyo, uwapo utaratibu ambao utaharakisha upatikanaji wa mikopo hiyo kwa kuwa kundi hili linahitaji uangalizi maalum tofauti na mikopo iliyotolewa kwa wale wasio na ulemavu," aliagiza.

Katika mkutano huo, Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Godwin Gondwe, alisema halmashauri yake imekuwa ikishughulikia masuala ya watu wenye ulemavu kupitia dawati la 'One Stop Jawabu' na halmashauri hiyo imekuwa ikitoa mikopo ya asilimia 10 (asilimia nne kwa wanawake, asilimia nne kwa vijana na asilimia mbili kwa watu wenye ulemavu) kwa ajili ya kuwainua kiuchumi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wanamichezo jipangeni kushindana na si kushiriki

**KWANZA** kabisa tunapenda kuwatakia kheri ya mwaka mpya Watanzania wote na hasa wadau wa michezo hapa nchini.

Ni jambo la kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufanikisha kuona mwaka mpya mwingine ambao leo umeingia katika siku ya pili.

Tukiwa bado tunasherehekea mwaka mpya, ni vyema tukatumia nafasi hii kukumbushana wanamichezo kuhusu majukumu mbalimbali ya kimataifa tuliyonayo.

Tanzania imekuwa ikishiriki katika mashindano mbalimbali ya kimataifa ya ikiwamo soka, ngumi, netiboli, riadha, kikapu, kuogelea na mingineyo.

Ni wazi kuwa kila mwanamichezo ndoto yake kubwa ni kushinda mataji makubwa na kujiweka katika historia kutokana na mafanikio ambayo atayapata.

Lakini ili kufikia ndoto hizo, ni wakati wa kila mhusika kuhakikisha anashiriki kikamilifu kwenye maandalizi ya msingi kwa lengo la kuvuna matokeo chanya.

Wote tunakumbuka mwaka jana tulikuwa na changamoto ya kuwapo kwa virusi vya corona ambavyo huleta ugonjwa wa COVID-19, ambao kwa kiasi kikubwa ulisimamisha mashindano na mazoezi mbalimbali ya michezo.

Kutokana na changamoto hiyo, kundi la wanamichezo liliathirika kwa kiwango kikubwa kutokana na kushindwa kutekeleza programu zake za mazoezi kikamilifu kwa sababu ya zuio la mkusanyiko wa pamoja lililotolewa na Serikali kupitia kwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Suala hilo limepita na sasa maisha yamerejea kama kawaida, hivyo muda wa kuandaa vyema timu na wanamichezo wetu (kwa wale wanaokwenda kushiriki mashindano ya mtu mmoja mmoja), umerejea hivyo tunatarajia kuwa na wawakilishi imara katika michuano yote watakayoshiriki.

Tunawakumbusha wanamichezo kuongeza umakini katika kujiandaa na mashindano kwa sababu mbalimbali na kuipeperusha vyema bendera ya Tanzania kimataifa, lakini hutoa nafasi kwa wanamichezo husika kujipatia zawadi mbalimbali ambazo husaidia kuongeza kipato au kumpaisha mhusika kwa kumpandisha hadhi.

Umefika wakati wanamichezo wa Tanzania wanapokwenda kushiriki mashindano ya kimataifa kufahamu wanatakiwa kwenda kupambana na si kusindikiza wengine.

Katika dunia ya sasa hakuna timu au mwanamichezo mdogo. Ukijiandaa vyema unaweza kupata matokeo mazuri na 'kuwafunika' nyota kutoka mataifa makubwa ambao mara nyingi huingia kwenye mashindano wakiamini kwamba tayari wao ni washindi.

Kujituma kwa wachezaji wa Kitanzania kutasaidia kulitangaza vyema jina la nchi, lakini pia kutarejesha heshima ya wanamichezo hao ambao kwa muda mrefu walionekana kuwa wasindikizaji au watu wanaokwenda kukamilisha ratiba kwa kutolewa mapema.

Tukumbuke hakuna kisichowezekana katika kusaka mataji, ukiwa na kikosi kilichoandaliwa vyema, matarajio ya kuvuna ushindi huwa ni makubwa na kwa sasa inawezekana kwa sababu tayari baadhi ya timu zimeonyesha kwamba Tanzania ya sasa ni moto.

Kwa mfano kwenye soka, timu zake tatu ambazo ni Timu ya Taifa (Taifa Stars), yenye wachezaji wa ndani imefuzu kushiriki fainali za Afrika (CHAN), Timu ya vijana ya umri chini ya miaka 20 na 17, zote pia zimekata tiketi ya kushiriki fainali za Afrika, hii haikutokea kwa bahati mbaya.

Mafanikio haya ambayo miaka ya nyuma ilikuwa ni nadra, yamepatikana na yanawezekana kulindwa kwa kuzipa maandalizi mazuri ya kwenda kwenye fainali hizo kushindana na si kushiriki kama ilivyozoeleka.

Tusiishie kufuzu, umefika wakati timu za Tanzania kufika hatua ya juu na pengine kushinda ubingwa wa Afrika kwa kujipanga kwenda kushindana na si kushiriki.

Mungu ibariki Tanzania, Mungu wabariki wanamichezo wote.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Tujihadhari na makocha Wazungu

Na Barnabas Maro

**"CHAKO** ni chako, cha mwenzako si chako." Maana yake kitu unachokiita chako ni kizuri na huweza kukufaa na una uhuru nacho kuliko cha mtu mwingine.

Methali hii yatufunza tuvitegemee vitu vyetu wala sio vya watu wengine. Pia hutukumbusha kuvithamini vitu vyetu ingawa sio vizuri kama vya watu wengine.

Kadhalika husemwa "Cha wenyewe huliwa na wenyewe." Maana yake kitu cha watu wengine huwafaidi wao wenyewe. Methali hii yaweza kutumiwa kuwahimiza watu wajitegemee badala ya kuwategemea wengine.

Mathias E. Mnyampala (Mungu amrehemu) aliandika kitabu kiitwacho 'Sikilizeni Hekima' chenye methali na mawaidha, kwamba: "Uchukivu hujificha katika ujanja; lakini shaurini ubaya wake huumbuliwa. Uchukivu huleta magomvi, lakini upendo huyafunika makosa yote."

'Ubaguzi' ni hali ya upendeleo katika kuwahudumia watu; sera au mpango wa kuhudumia watu kwa kuegemea misingi ya hadhi, kabila, elimu, rangi n.k. Wazungu ni weupe wenye nywele ndefu, laini za singa, tofauti na Waafrika wenye nywele nyeusi tena ngumu.

Kwa ujinga wetu, twadhani kila kifanywacho na Wazungu ni maendeleo, hivyo twapaswa kuiga kila wafanyacho kumbe twajidhalilisha.

Baadhi ya mambo ya kijinga wafanyayo Wazungu, sisi twaiga kwa dhana kuwa ndio 'maendeleo' kumbe ni ujinga uliopituka (kitendo cha kurudia kupita mahali pale pale mara nyingi!) Mfano ni wasichana wetu kuvaa suruali zilizochanwa magotini, au kuvaa nguo fupi zinazoonyesha sehemu nyeti za miili yao. Wavulana hutoga ndewe (sehemu ya chini ya sikio iliyo duara) ili kuvaa hereni, kuwa na kucha ndefu, kuzipaka rangi na nywele ndefu zilizosukwa, kwa dhana kuwa ndio 'maendeleo.'

Baada ya kueleza hayo, sasa nauliza: Tunawathamini Watanzania wanaotoa mafunzo ya michezo, wakufunzi wa michezo, yaani makocha wetu wa kandanda? Jibu la moja kwa moja ni hapana! Tunao makocha wengi wazuri, lakini tunashindwa kuwaendeleza na kuwatumia kwani hatuwathamini! Badala na kuwatumia twawakimbilia Wazungu na kuwalipa fedha nyingi na masilahi mazuri kuliko makocha wetu, ndio maana wanatudharau na kutuona sisi si binadamu kama wao!

Hatujifunzi kwa yale yatokeayo Marekani na Ulaya ambako baadhi ya Wazungu huwafananisha Waafrika na nyani? Wenye runinga wameona jinsi baadhi ya wachezaji Waafrika wanavyolinganishwa na nyani ingawa wamesajiliwa na timu za Wazungu wanaojua ubinadamu!

Ina maana Tanzania haina wachezaji mahiri wanaojua kulichezea 'gozi la ng'ombe nyama kala nani?' Hasha! Tuna takriban wachezaji 20 wanaocheza mpira katika nchi mbalimbali za Afrika, Marekani na Ulaya lakini tumeshindwa kuwatumia. Hivyo wakaamua kwenda ughaibuni wanakozidisha ubora wao wa kucheza na kulipwa fedha nyingi kuliko walizokuwa wakilipwa huku nyumbani.

Yanga, Simba na Azam ndizo timu zenye mazoea ya kuajiri makocha wa ughaibuni, hasa Wazungu. Hata hivyo hawadumu kwa muda mrefu katika timu hizo. Sababu ni kushindwa kuziendeleza timu, kuwadhalilisha wachezaji kwa kuonesha ubaguzi wa rangi na kutowatii viongozi ambao ndiwo waliowaajiri!

Mwaka jana, Simba na Yanga ziliwafukuza makocha wao kwa kutowatii viongozi wa vilabu na kuwadharau makocha wasaidizi na wachezaji. Sababu hizo ziliwafanya washindwe kuleta maendeleo ya timu zao wakionesha wazi ubaguzi wa rangi. Kwa nini waajiriwa wawadharau waajiri wao na watu wanaofanya nao kazi? Ualimu ni kazi ya kutoa taaluma kwa watu; usomeshaji.

Makocha Wazungu waliofukuzwa Yanga na Simba mwaka jana ni sababu ya kuwadharau makocha wenyeji na kutoelewana. Hivi karibuni nilishituka niliposoma kwenye gazeti la michezo jinsi kocha wa moja ya timu hizo kutotaka kuwaona viongozi wakuu kwenye mazoezi ya timu husika! Viongozi wanataka kuona ufundishaji wake na jinsi wachezaji wanavyofuata mafunzo lakini kocha hataki uwepo wao! Kama kocha huyo ni hodari sana mbona hakupata ajira kwao mpaka akaja Tanzania kwa watu weusi wanaomlipa mshahara mkubwa lakini anawadhau?

Ni vyema timu zenye uwezo kuwa na utaratibu wa kuanzisha shule za makocha wa kandanda na michezo mingine inayochezwa duniani, au kuwapeleka baadhi ya makocha kwenda kujifunza zaidi nchi zingine ili tuwe na makocha wetu badala ya kuwategemea wageni wasiokuwa na fadhila wala adabu.

# HABARI PICHANI



Wachuuzi wa kuku Soko la Buguruni jijini Dar es Salaam, wakiwashusha katika gari kwa ajili ya kuwauzia wateja, kuku mmoja aliuzwa kwa Sh. 5,000 kwa bei ya jumla jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Mfanyabiashara wa mananasi katika soko la Buguruni jijini Dar es Salaam, akiliandaa nanasi kwa kuuza kipande kimoja kwa shilingi 200. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Ofisa Maendeleo ya Jamii Manispaa ya Temeke, Devotha Nchia, akitoa taarifa kuhusu utekelezaji wa utoaji wa mikopo kwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Wenye Ulemavu, Ummy Nderiananga (hayupo pichani), wakati wa kikao kazi hicho.



Watumishi wa Shirika la Umeme nchini (TANESCO) wakifuatilia maelekezo yaliyotolewa na Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, wakati wa kikao kazi cha waziri huyo na watumishi wa TANESCO Mkoa wa Shinyanga, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**




Wanamichezo wa kikundi cha mazoezi ya viungo mkoani Dodoma, wakishiriki katika Tamasha la Mazoezi ya Viungo la Kitaifa Zanzibar, huku wakipita katika jukwaa kuu la viongozi wakati wa kumalizia matembezi hayo na kupokelewa na Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi. **PICHA: IKULU**



Kamishna wa Utawala na Fedha wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Mbaraka Semwanza (katikati), akiongea na maofisa, askari na watumishi wa kada nyingine (hawapo pichani), alipokuwa kwenye kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa Makao Makuu mkoani Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DAWASA watamba kuongeza makusanyo

**Na Crispin Gerard**

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) Mkoa wa Huduma Mabwepande jijini Dar es Salaam, imejipanga kuongeza makusanyo ya mkoa kutoka Sh. milioni 200 hadi Sh. milioni 400 kwa mwezi.

Mpango huo unaenda sambamba na uboreshaji wa miundombinu ya kusambaza maji kwa wateja waliopo na wateja wapya wanaotarajiwa kusajiliwa hivi karibuni.

Akizungumzia mipango ya mkoa wake wa kihuduma, Meneja wa DAWASA Mabwepande, Haruna Taratibu, alisema kwa sasa mkoa wa Mabwepande unahudumia wakazi wapatao 9,400 waliosajiliwa na kwamba mapato yatokanayo na makusanyo kwa mwezi ni wastani wa Sh. milioni 200.

Taratibu alisema mkoa huo zao la Mkoa wa DAWASA Tegeta uliogawanywa sehemu mbili na kutengeneza mikoa ya DAWASA Mabwepande na DAWASA Mivumoni.

Alisema Mkoa wa DAWASA Mabwepande unahudumia kata mbili ambazo ni Bunju na Mabwepande.

"Kata ya Bunju ina mitaa sita na mkoa wa DAWASA Mabwepande unahudumia mitaa mitatu ambayo ni Kilungule, Bunju A na Bunju Mkoani, huku Kata ya Mabwepande ikihudumia mitaa mitano ambayo ni Bunju B, Kihonzile, Mabwepande, Mji Mpya na Mbopo.

"Kama mkoa mpya wa kihuduma, tumeweka mikakati mbalimbali ya kuhakikisha tunaongeza makusanyo na kuboresha huduma zaidi, mkakati mmojawapo ni kudhibiti maji yanayopotea njiani," alisema.

Kwa hatua za awali, tumejigawa katika kanda tatu ili kuhakikisha tunawafikia wateja wengi zaidi na kudhibiti upotevu wa maji.

"Tunaamini kwa kuzuia upotevu wa maji, tutaweza kuimarisha upatikanaji wa maji kwa kuelekeza maji yanayopotea kwa wakazi wasio na maji," alisema.

Alisema mipango iliyowekwa na Mkoa wa DAWASA Mabwepande kwa mwaka 2021/22 ni kuhakikisha ankara sahihi za wateja zinawafikia ikiwa na kukusanya madeni baada ya kuyahakiki.

"Sehemu ya madeni kwa wateja wetu ni madeni ya mikopo ya kuunganishwa huduma kwa mara ya kwanza, tumeanzisha utaratibu wa kuingia mkataba na wananchi kwa kulipa madeni yao kidogo kidogo kila mwezi mpaka wamalize," alisema.

Alitoa wito kwa wananchi wanaopata huduma ya maji kushirikiana na mamlaka kwa kutoa ushauri, maoni na kero ili kuboresha huduma.

Mkoa wa kihuduma Mabwepande unatumia chanzo cha maji cha Ruvu Chini na unahifadhi majisafi kwenye tangi lenye uwezo wa kubeba lita milioni sita za maji lililoko Marolo.




Meneja wa Tigo Kanda ya Pwani, Robert Kasulwa (kushoto), akimkabidhi funguo za pikipiki, Josephine Joseph, wa Dar es Salaam baada ya kuibuka mshindi kwenye kampeni ya 'Jaza Tukujaze Tena' iliyofanyika juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wananchi walia kupokwa shamba na viongozi wao

**Na Mary Mosha,** MOSHI

BAADHI ya wananchi wa Kata ya Kibosho, Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro, wameulalamikia uongozi wa Tarafa ya Kibosho, kwa kutaka kuwaondoa kwenye shamba lao.

Wamelidai shamba hilo walikabidhiwa na serikali baada ya kutoa maeneo yao kwa ajili ya kupisha ujenzi wa Shule ya Sekondari Kirima.

Mbali na mpango wa kuwaondoa katika eneo hilo, pia wamelalamikia kitendo cha kuharibiwa kwa mazao yao yaliyokuwa shambani.

Akizungumzia mgogoro huo, Bonaventure Kimaro, mmoja wa walazi hao, alisema kuwa mwaka 1999, wananchi waliokuwa wakiishi karibu na shule za msingi na sekondari Kirima, shule za msingi za Masoka, Mangikida chini, Singabora na Kituo cha Polisi Kirima, walitakiwa kutoa maeneo yao ili kupisha upanuzi na ujenzi wa shule hizo na serikali ilitoa ekari 37 kwa wananchi hao kama fidia.

Alisema eneo lililotolewa, lilikuwa na ukubwa wa ekari 154, zilizokuwa za Chama cha Ushirika cha Kilimaboro na kati ya ekari hizo, ekari 117 alipewa mwekezaji wa Vassol Agrovet, kampuni inayojihusisha na kilimo cha maua kwenye kata hiyo.

Hata hivyo, mwaka 2005 wananchi ambao hawakufahamika, walivamia shamba hilo na kukata migomba ambayo ilikuwa shambani huko kwa madai kuwa shamba hilo limevamiwa na watu wasiojulikana.

"Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Moshi kwa wakati huo, aliingilia kati na kusuluhisha tatizo hilo, lakini mwaka 2009 watu walivamia tena mashamba hayo, hali iliyosababisha kwenda mahakamani na walishinda kesi na kurudi kwenye maeneo yao waliokabidhiwa na serikali," alisema. Paulo Lemensi, mkazi mwingine wa eneo hilo, alidai kuwa Oktoba 5 mwaka jana, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Kirima na Ofisa Tarafa ya Kibosho, walifika katika mashamba hayo na kutoa tangazo la katazo kwa wananchi kutofanya shughuli yoyote katika mashamba hayo, jambo ambalo limesababisha kuwa na hofu ya hatima ya eneo hilo.

Alisema kuwa baada ya tangazo hilo, wakati wakitafuta suluhisho la eneo hilo, Desemba 4 mwaka jana, watendaji wa serikali walifika tena kwenye mashamba hayo wakiwa na mwekezaji wanaliyepakana naye na walipitisha trekta na kulima mazao ya wananchi ambayo yalikuwa shambani.

"Mwekezaji huyu kuna kitu anatafuta, anataka kuchukua eneo hili ambalo Rais ameruhusu litumike kwa ajili ya ujenzi wa shule," alisema Kimaro.

Diwani wa Kibosho Kati, Bahati Mamboma, alisema baada ya tangazo la kuzuiwa kwa wananchi kuingia katika eneo hilo, waliwataka kuwa watulivu ili kutoa nafasi viongozi kulishughulikia tatizo hilo.

Evarista Kulawa, mkulima katika shamba hilo, alisema amekuwa akilima katika shamba hilo kwa kukodishiwa.

Alisema kitendo kilichofanywa na mwekezaji huyo, kuharibu mazao yaliyokuwa shambani, kimewaumiza kwa kuwa familia zao zinategemea chakula kutoka kwenye shamba hilo.

Akijibu tuhuma za wananchi hao, Ofisa Tarafa ya Kibosho, Yusuph Munisi, alisema baada ya Chama cha Ushirika kutoa eneo kwa ajili ya wananchi waliotoa maeneo yao kupisha ujenzi wa shule hizo, haikufanyika hivyo na tukio hilo lilisababisha mgogoro wa muda mrefu.

"Lengo la kuweka katazo ni ili wananchi wajitokeze na waeleze fidia waliyopewa na tuzungumze na kila mmoja aliyekuwa na eneo kwenye shamba hilo, ili kama wapo kihalali, wapewe na kumaliza mgogoro huu.

"Kabla ya kwenda, nilipewa maelekezo kutoka kwa Mkuu wa Wilaya kwa kuwa mgogoro huu anaufuatilia kwa karibu kuhakikisha unamalizika," alisema.

Akitoa msimamo wa serikali kuhusu ya mgogoro huo, Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Alhaji Kundya, alisema suluhisho la mgogoro huo ni kutafuta uhalali wa wananchi waliokuwa kwenye shamba hilo.

"Hatupendi mtu yeyote apoteze haki yake, tunataka mkataba ulioingiwa kati ya halmashauri na mwekezaji wa shamba uwe mkataba ambao hautakuwa na mgogoro, ili mwenye hati ya shamba hilo, aweze kuliendeleza.

# Waziri aagiza kasi iongezwe usambazaji umeme migodini

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, ameliagiza Shirika la Umeme (TANESCO) kuongeza kasi ya usambazaji umeme kwenye maeneo ya migodi midogo ya uchimbaji wa madini.

Amesema kwa kufanya hivyo, watawapunguzia gharama kubwa ambayo wanaitumia kuzalisha madini kutokana na kutumia mafuta mazito kuendesha mitambo ya kufua umeme.

Dk. Kalemani alitoa agizo hilo, juzi, alipofanya ziara ya kutembelea mgodi mdogo wa uchimbaji madini ya dhahabu Nyangalata ulioko wilayani Kahama mkoani Shinyanga, na kujionea namna wachimbaji hao wanavyotumia gharama kubwa ya kuendesha mitambo ya kufua umeme kutokana na kutumia mafuta mazito.

Alisema Rais John Magufuli ameshatoa fedha, ili wananchi wapatiwe huduma ya umeme yakiwamo maeneo ya migodi midogo.

Aliagiza TANESCO kuhakikisha kuanzia kesho Januari 2, wazuru kwenye mgodi huo wa Nyangalata, ili wawauganishie umeme haraka na kuongeza kasi ya uzalishaji madini. "Lengo la Rais ni kuwakuza wachimbaji wadogo, ili wachimbe madini kwa ufanisi, kuongeza kasi ya uzalishaji madini na kukua kiuchumi na taifa kwa ujumla.

"Wakitumia nishati ya umeme, wataokoa gharama za uzalishaji kwa asilimia 80, ambayo wanaingia kwa sasa kutokana na kutumia mafuta mazito kuendesha mitambo ya kufua umeme," alisema.

Waziri huyo alisema serikali imepanga kuanzia Februari 5 mwaka huu, usambazaji wa huduma ya umeme kwenye vitongoji ianze nchi nzima.

Alionya TANESCO kwamba ni marufuku kumuuzia mwananchi nguzo ya umeme na akishalipia fedha ndani ya siku saba awe ameshauganishiwa umeme.

Akiwa katika kituo cha kupokea umeme, kusambaza na kupoza kilichoko Bulyanhuru wilayani Kahama, alikazia agizo lake la kutokata umeme ovyo.

Mbunge wa Msalala, Iddi Kasimu, alisema kasi ya usambazaji umeme kwenye makazi ya watu na maeneo ya migodi, itakuwa ni kichocheo kikubwa cha ukuaji wa maendeleo kwa wananchi na wachimbaji wadogo.

Mmoja wa wachimbaji wadogo kutoka mgodi huo wa Nyangalata, Alex Manyama, alisema kutokana na kutumia mafuta mazito kuendesha mitambo ya kufua umeme na kuzalisha madini, wamekuwa wakitumia kwa siku Sh. 900,000, hivyo kuiomba serikali iwapelekee haraka huduma ya umeme.



# Tume ya Ushirika yaagizwa kasi utoaji leseni SACCOS

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

TUME ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), imeagizwa kuongeza kasi ya kushughulikia maombi ya leseni na utoaji wake kwa vyama vya ushirika wa akiba na mikopo (SACCOS).

Agizo hilo lilitolewa jana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya, alipokuwa akikabidhi kompyuta 50 zilizotolewa na Benki ya CRDB kwa tume hiyo.

Kusaya alisema matarajio ya serikali ni kuona kompyuta hizo zinaongeza kasi ya uwajibikaji kwa watumishi wa tume hiyo ikiwamo kutoa leseni na utendaji kazi wao utapimwa kupitia vifaa hivyo.

"Itakumbukwa kuwa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Namba 10 ya mwaka 2018 pamoja na kanuni zake za mwaka 2019, zinaelekeza kila mtoa huduma ndogo za fedha nchini, zikiwamo SACCOS, kutakiwa kuomba leseni kwa mujibu wa sheria hiyo," alisema.

Alisema kutolewa kwa kompyuta hizo kutasaidia ofisi kusimamia utoaji wa leseni ambazo zinaombwa na kutolewa kwa njia ya mtandao.

"Mnapaswa kuongeza ufanisi katika upatikanaji, utunzaji na utoaji wa taarifa na takwimu mbalimbali za vyama vya ushirika kama vile idadi ya vyama, wanachama, hisa, mtaji, ukaguzi, usajili, uwekezaji, masoko, madeni na migogoro," alisema.

Aliitaka tume hiyo kuhakikisha inatunza ipasavyo na kutumika vizuri ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

"Watumishi walikuwa hawana vitendea kazi kama kompyuta na hivyo kushindwa kufanya kazi zao kwa ufanisi uliohitajika, baada ya kukabidhiwa kompyuta hizi, utendaji na ufanisi wa kazi zao utathminiwe mara kwa mara na itakapothibitika kushindwa kufanya kazi zao kwa uharaka, ufanisi na weledi kwa kutumia vifaa hivi hatua zichukuliwe," alisema.

Aliishukuru CRDB kwa vifaa hivyo, huku akitoa wito kwa taasisi na mashirika mengine kuiga mfano huo wa kutoa sehemu ya mapato yao kununua kompyuta hizo.

Kuhusu kuwachukulia hatua wanaohujumu ushirika, Kusaya aliitaka tume kuendelea kuchukua hatua kwa viongozi wa vyama vya ushirika wanaohujumu.

Mtendaji Mkuu wa Tume hiyo na Mrajis wa Vyama vya Ushirika nchini, Dk. Benson Ndiege, alisema kukosekana kwa vitendea kazi. zikiwamo kompyuta na vyombo vya usafiri, kumesababisha vyama vya ushirika kutokaguliwa mara kwa mara.



Wasamaria wema wakimsaidia kushusha tenga la nyanya kijana mbeba mizigo anayefanya shughuli zake kwenye soko kuu la Majengo, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Waziri Jafo akunwa na utendaji Bahi

**Na Paul Mabeja,** BAHI

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, ameipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Bahi mkoani Dodoma kwa usimamizi mzuri wa fedha za serikali katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Jafo alibainisha hayo jana wakati alipotembelea utekelezaji wa miradi katika halmashauri hiyo na kutumia fursa hiyo kuzungumza na watumishi

"Bahi nimefarijika sana na watumishi wa hapa hususani usimamiaji wa fedha za miradi mbalimbali kama elimu na afya, hata matumizi ya fedha yameonekana.

"Awali nilipokuwa nakuja hapa palikuwa pa tofauti. Watu walikuwa na nyuso za huzuni, lakini sasa hivi halmashauri hii inafanya vizuri zaidi, lakini mnapofanya mabadiliko mahali popote si watu wote wanafurahi," alisema.

Waziri Jafo alisema Bahi wamemfurahisha kwa kazi nzuri ya utekelezaji miradi mbalimbali ya maendeleo kwa kutumia fedha za serikali, ili kuwezesha wananchi wapate huduma nzuri.

"Bahi mna 'good performance' (utendaji mzuri), hivyo endeleeni kufanya kazi. Mimi sitaki kila mtu nikija hapa awe anatafuta pa kutokea.

Nataka kila mtu awe na amani na mtu akikosea awajibishwe kwa mujibu wa sheria," alisema.

Pia alisema watumishi wanatakiwa hata wakitaka kuondoka eneo fulani, watu wajiulize kwa nini anaondoka eneo hilo ikiwa na maana kuwa ni mtumishi bora na umuhimu wake unaonekana.

"Fanya kazi acha 'legacy' (alama) mahali unapofanya kazi ili watu wakukumbuke na si ukiondoka wanasema afadhali ameondoka. Hilo si jambo zuri, sipendezwi unamwambia mtu akuandikie amefanya nini mwaka mzima lakini hawezi," alisisitiza Jafo.

Alisema kila mtu akisimamia eneo lake vizuri atapata heshima kubwa, huku akijitolea mfano kuwa yeye alikuwa fundi seremala, lakini baada ya kumaliza chuo alikuwa bwana shamba na aliajiriwa kwa kazi hiyo, lakini hadi leo anakumbukwa kule sababu aliacha alama.

"Fanyeni kazi tukijua kuwa Mungu amewateua nyie kuhudumia wananchi wanyonge, sisi viongozi tuna tabia ya kutopendana wakati mwingine kuna wakuu wa idara wanaona watu wa chini yake ni vikaragosi hali inayofanya watu wafanye kazi kwa huzuni.

"Acheni kunyanyasa viongozi wa chini, acheni kupandisha mabega juu, acheni kujikweza, acheni kiburi katika kazi kwa sababu maisha hayana Formula huwezi jua kesho unayemdharau atakuwa nani," alibainisha Jafo.

## REA yawakumbuka yatima Mwaka Mpya

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MENEJIMENTI na wafanyakazi wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), wametoa misaada mbalimbali yenye thamani ya Sh. milioni 10 katika vituo viwili vya kulelea watoto yatima na wenye ulemavu jijini Dodoma kusherehekea Mwaka Mpya.

Vituo vilivyopatiwa misaada hiyo ni Miyuji na Kituo cha Yatima cha Rahman.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa REA wakati wa kukabidhi misaada hiyo kwenye vituo hivyo, Ofisa Uhusiano wa REA, Jaina Msuya, alisema wametoa misaada hiyo ili watoto hao washerehekee sikukuu hiyo kama wengine.

Msuya alisema miongoni mwa vitu walivyovitoa ni vyakula, vinywaji, mbuzi na vifaa vya shule vya wanafunzi yaiwamo madaftari na peni ili viwasaidie kipindi shule zitakapofunguliwa.

"Tumeamua kutoa misaada hii ikiwa ni kuonyesha kuwa tunawathamini hawa watoto pia nao washerehekee sikukuu ya mwaka mpya vizuri, tumetoa vyakula, vinywaji na haya madaftari yawasaidie watoto shule zitakapofunguliwa," alisema Msuya.

Mbali na misaada hiyo pia walitoa Sh. milioni 1.2 kwa kila kituo kwa ajili ya kununua mahitaji mengine.

Pia alisema REA wataendelea kushirikiana na vituo ili watoto hao wapate faraja na kujiona ni miongoni mwa jamii.

Msuya aliwahimiza watu binafsi, mashirika na taasisi mbalimbali kuona haja ya kusaidia vituo kama hivyo ambavyo vinalea watoto yatima na wenye ulemavu.

Mlezi wa kituo cha Miyuji, Sister Aurea Kyara, alishukuru REA kwa misaada hiyo na kubainisha kuwa itakwenda kusaidia katika malezi ya watoto na watafarijika.

Sister Aurea aliwahimiza wadau wengine kujitokeza kuwasaidia watoto na kuona jukumu hilo ni lao ili watoto wapate upendo na faraja.

Naye Msaidizi wa Rahman Orphanage Centre, Aisha Mohamed, alishukuru REA kwa msaada huo na wanawaombea Mungu awabariki kwa kile walichotoa kwa watoto hao.



# Ahimiza kasi vita vitendo vya ukatili

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amesema jamii inaweza kuendelea kubakia salama endapo itakubali kutafakari kwa kina jinsi ya kuvitafutia dawa vitendo vya udhalilishaji vinavyoonekana kuwaathiri zaidi wanawake na watoto.

Amesema serikali tayari imejizatiti pamoja na mambo mengine, kufanya mabadiliko ya baadhi ya sheria za kudhibiti vitendo hivyo viovu na kuitaka jamii, hasa viongozi wa taasisi za kiraia, kuelekeza nguvu katika kuondokana na kadhia hiyo.

Akizungumza jana na viongozi wa Jumuiya ya Maimamu Zanzibar (JUMAZA) ofisini kwake, Vuga mjini Zanzibar, Hemed alisema inasikitisha kuona ongezeko la vitendo vya udhalilishaji na kutia huzuni zaidi kuona miongoni mwa wafanyaji wa uovu huo ni wazee wa zaidi ya miaka 70.

Hemed alisema nguvu za pamoja baina ya viongozi na wananchi hasa katika ngazi ya shehia na jimbo katika utoaji wa ushahidi dhidi ya watu wanaotuhumiwa kujihusisha na vitendo vya udhalilishaji zinatakiwa.

Aliwataka viongozi kuwahamasisha wananchi kujenga tabia ya kutoa ushahidi pale wanaposhuhudia matukio ya vitendo hivyo. Kinyume na hatua hiyo, alisema ni sawa na kusema hakuna hatua itakayokuchukuliwa na wasimamizi wa sheria.

Makamu wa Pili huyo alionya kwamba kiongozi yeyote atakayeshikwa kwa vitendo vya udhalilishaji serikali itamhesabu kama mhalifu na atalazimika kuchukuliwa hatua za kisheria bila ya kujali dhamana aliyokabidhiwa.

Mtendaji Mkuu huyo wa shughuli za serikali aliitaka jamii kubeba jukumu na dhima ya kuhakikisha kizazi kipya kinajikita katika kujitafutia elimu.

Alisema wako wanafunzi wenye uwezo mkubwa wa ufahamu, lakini baadhi yao tayari wameshajengwa vibaya na matokeo yake huathiri ukosefu wa wataalamu kutokana na kundi kubwa kuelekea kwenye fani moja.

"Miaka 10 iliyopita tumeshuhudia hali ya kutisha iliyofikia wakati anatafutwa mwanafunzi wa fani ya sayansi anakosekana na kulazimika kutumia nguvu za ziada katika kuwaandaa ili kukidhi mahitaji halisi," alisema Hemed.

Viongozi wa Jumuiya ya Maimamu Zanzibar walisema katika kukabiliana na mporomoko wa maadili katika jamii wamelazimika kuanzisha chuo cha mafunzo ya ndoa kwa lengo la kurejesha hazina hiyo ya maadili.

Kaimu Katibu wa Jumuiya hiyo, Sheikh Ali Abdalla Amour, alisema yako matukio mengi ya ajabu miongoni mwa jamii hasa vijana yanayotishia hatima mbaya ya jamii, jambo ambalo litapelekea kuikosesha serikali kupata nguvu kazi ya baadaye.



Washiriki wa Tamasha la Mazoezi ya Viungo Kitaifa Zanzibar, Pili Mwalimu (kulia) na Kazija Othman, wakimaliza matembezi ya tamasha hilo, huku wakipita katika jukwaa kuu la viongozi Uwanja wa Amaan, Zanzibar. Matembezi hayo yalianzia viwanja vya Mapinduzi Square Michezani Kisonge na kumalizia Uwanja wa Amaan kwa mazoezi ya pamoja. **PICHA: IKULU**

# Ateuliwa mwanamke wa kwanza

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, amemteua Zena Ahmed Said, kuwa Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ).

Zena ambaye anakuwa mwanamke wa kwanza kushika wadhifa huo, anatarajiwa kuapishwa leo katika hafla itakayofanyika Ikulu, Zanzibar.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi Ikulu Zanzibar, Zena anachukua nafasi iliyoachwa wazi na Dk. Abdulhamid Yahya Mzee ambaye amestaafu utumishi wa umma.

Dk. Abdulhamid amefanya kazi na marais wastaafu Amani Abeid Karume na Dk. Ali Mohamed Shein na kumalizia utumishi wake akiwa na Rais Dk. Mwinyi akiwa katika wadhifa huo. Kabla ya uteuzi huo, alikuwa Katibu Mkuu Wizara ya Nishati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na alishawahi kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Tanga.

Akizungumza na Nipashe kuhusu uteuzi huo, Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, alimpongeza Rais Mwinyi kwa kuwapa kipaumbele wanawake hasa katika nafasi hiyo ambayo haijawahi kushikiliwa na mwanamke.

"Nimefurahi sana kwa sababu nafasi hiyo inahitaji mtu mwenye uwezo wa kuangalia bila ya ubaguzi, na yeye kwa kuwa ni mkuu wa utumishi, tuaamini ataweka mfumo mzuri wa ajira kwa mujibu wa mtu wa taaluma yake na si kwa ujamaa. Naamini atasaidia sana idara ya utumishi kupata mabadiliko," alisema.

Pia alisema anaamini kiongozi huyo ataleta nidhamu kubwa ya utendaji ili ripoti za serikali ziwe zinapatikana.

Dk. Mzuri alisema wanawake wana uwezo mkubwa, hivyo ataleta mabadiliko mazuri serikalini hasa ikizingatiwa ni msomi mzuri.

Mwishoni mwa mwaka jana, alipotangaza baraza lake la mawaziri, Rais Mwinyi alisema hatakuwa na ubaguzi wowote hasa wa kijinsia katika kuteua nafasi mbalimbali za uongozi.

Pia alisisitiza kuwa atateua watu kwa mujibu wa sifa, elimu na uwezo wa mtu kufanya kazi ambaye ataendana na kasi yake.

# Mwinyi ataka vitendo zaidi mwaka 2021

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, amewataka wananchi kuuanza Mwaka Mpya wa 2021 kwa kufanya kazi kwa ari na kuiunga mkono Serikali ya Umoja wa Kitaifa, ili kutekeleza majukumu yake iliyojipangia kwa wananchi.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana katika salamu za Mwaka Mpya kwa wananchi wa Zanzibar kupitia vyombo vya habari.

Aliwataka wananchi kuiunga mkono serikali katika juhudi zake za kupambana na rushwa, kuongeza kasi ya uwajibikaji katika sehemu za kazi, ili kuleta ufanisi na kuyafikia malengo ya uchumi na uwekezaji.

Uzembe, ubadhirifu na rushwa, alisema havitavumiliwa katika kipindi cha uongozi wake na kuwataka wananchi kumuunga mkono katika kutokomeza vitendo hivyo.

"Uchaguzi umekwisha na tayari tumeunda serikali na inafanya kazi zake. Nawaomba wananchi watuunge mkono katika mambo ambayo tumeona yamekuwa kero kwa wananchi na kusababisha watu wachache kujinufaisha kwa maslahi binafsi," alisema.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa, alisema imeundwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na kwamba kati ya malengo yake makubwa ni kuimarisha umoja, mshikamano na utulivu wa nchi.

Alisema matarajio yake ni wananchi wa Zanzibar kupata mafanikio makubwa katika ngazi mbalimbali zikiwamo uchumi na maendeleo pamoja na kisiasa.

Dk. Mwinyi alisema mwaka 2020 umeacha majonzi makubwa baada ya jengo la kihistoria lililobeba sura ya Zanzibar la Beit-al-jaib, kuanguka na kusababisha maafa ya watu wawili kufariki dunia na wengine wanne kujeruhiwa.

Alisema serikali itafanya juhudi zake zote kuhakikisha kwamba jengo hilo linarudi katika sura na uhalisia wake kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za kimataifa.

Pia alisema katika mwaka 2020 dunia, ikiwamo Zanzibar, ilikumbwa na janga kubwa la ugonjwa wa corona na kusababisha athari kubwa za kiuchumi.

Alisema uchumi wa Zanzibar umeathirika kwa kiwango kwamba nchi za visiwa uchumi wake mkubwa ni utoaji wa huduma na sekta ya utalii.

Hata hivyo, Dk. Mwinyi alisema katika kipindi cha mwaka 2020 Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepata mafanikio makubwa ya kiuchumi chini ya Rais John Magufuli kwa Benki ya Dunia kuitangaza Tanzania kuingia katika uchumi wa kati hatua ambayo inatia moyo ya kuwapo kwa mafanikio makubwa katika uongozi wa nchi.

"Matarajio yangu tutapata mafanikio makubwa ya kiuchumi na maendeleo kwa ushirikiano wa uongozi wa pamoja kati ya serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Rais Dk. John Magufuli na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar," alisema.



**WEUSI WA OFFICIAL NINI BURUDANI TOSHA** Ukurasa 12



Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE



## 'LOVE STORY 2020'

# Mapenzi yalinoga, yaliliza mastaa

NI wazi kati ya vitu ambavyo vilichukua nafasi miongoni mwa mastaa wa Bongo mwaka 2020 ni mapenzi.

Ndani ya mwaka huo ambao ulifikia tamati yake juzi, na sasa tupo katika mwaka mpya wa 2021, baadhi ya mastaa walijikuta wakiingia katika mapenzi mazito na wengine walitokwa na machozi ya machungu baada ya penzi lao kufikia mwisho.

Baadhi ya wasanii waliojikuta wakichukua maamuzi mazito ya kuachana na sanaa na wengine kubadili dini kutokana na kuzidiwa na mahaba kwenye mioyo yao.

Wafuatao ni baadhi ya mastaa waliojikuta mapenzi yakisababisha kuchukua hatua mbalimbali.

**VANESSA MDEE**

Wiki ya mwisho ya 2020 Vanessa amevalishwa pete ya uchumba na Rotimi ambaye ni msanii wa filamu nchini Marekani.

Kabla ya kufikia hatua hiyo, Vanessa alitangaza kuachana na muziki na badala yake kuamua kuishi na mpenzi wake nchini humo, huku akidai hatua yake hiyo ni kutaka kupumzisha akili na kufanya shughuli zingine.

Kupitia video fupi ambazo zimesambazwa kwenye mitandao ya kijamii, zimemwonyesha Rotimi akiwa amepiga magoti mbele ya Vanessa huku akimvalisha pete hiyo ya uchumba.

Alipomaliza kumvisha, wapenzi hao walikumbatiana na kisha kupeana mabusu motomoto.

**SHILOLE**

Msanii mwingine wa kike ambaye mwaka 2020 alijikuta akilia na kutabasamu kutokana na mapenzi ni Shilole. Akitumia falsafa yake ya kuwa na wapenzi vijana wadogo, Shilole aliachana na mume wake Uchebe huku ikiambatana na kilio.

Mwanamuziki huyo ambaye pia mjasiriamali, alionekana kuwa hayuko sawa baada ya kuachana na mume wake, lakini miezi ya mwisho ya mwaka huo alianza uhusiano wa kimapenzi na Romy, ambaye pia ana umri mdogo kuliko yeye.

**NANDY NA BILNASS**

Baada ya kuwapo kwa uvumi kuwa wasanii wa Bongo Fleva, Nandy na Bilnass ni wapenzi, hatimaye mwaka 2020 ukweli ulibainika na wawili hao walitangaza wapo katika mahaba mazito.

Katika kuhakikisha wanachokifanya sio siri tena, waliamua kuvishana pete ya uchumba, lakini mpaka sasa hawajatangaza lini wanaweza kufunga ndoa.

**BEN POL**

Katika jambo ambalo liliwashtua wadau wa muziki nchini, ni hatua ya mwimbaji maarufu wa R&B nchini, Ben Pol kubadilisha dini.

Katika ujumbe wake wa Oktoba 23 kwenye ukurasa wake wa Instagram, alitangaza kuwa amebadili dini na kuwa Muislamu. sasa atatambulika kwa jina Behnam Paul Mnyang'anga, badala ya Benard la awali.

Hata hivyo, uamuzi wake huo unaeleza unatokana na kutawaliwa na mapenzi baada ya kumpata mwanamke mwenye imani ya dini hiyo.

BASI SAWA

## Mpoto awashukia wasanii wabagua misiba

BINGWA wa muziki wa kughani mashairi, Mrisho Mpoto, amesema wananchi wamekuwa na maswali magumu kuhusu tabia za wasanii wa bongo kuchagua misiba.

Amesema si jambo zuri kwa kuulizwa maswali hayo, lakini inabidi watu kuuliza kutokana na baadhi ya wasanii kubagua misiba kwa kuchagua ile ambayo wataweza kujitangaza na kuacha ile ya kawaida.

"Swali hili linasikitisha, lakini watu wanauliza kwa kile wanachokiona, ni lazima sasa tujitambue kwa kwenda katika misiba ya aina yote badala ya kuchagua ipi wanaenda na ipi hawaendi," amesema Mpoto.





## D Rhymes awaambia 'You Body Shake'

MWANAMUZIKI chipukizi wa Bongo Fleva, Denis Kasaba, maarufu kama D Rhymes Tz, ametambulisha video ya ngoma yake mpya 'Your Body Shake' ambayo tayari umeanza kutikisa anga la muziki.

Wimbo huo ambao upo kwenye mtandao wa You Tube, imetayarishwa na Prodyuza Dimoo Records na video yake imefanywa chini ya muongozaji Mwene.

"Wimbo wangu unazungmzia mapenzi, lakini unachezeka vizuri kitu ambacho inawafanya watu kupenda kuuzikiliza kila wakati," amesema nataka.



## HAYAKUHUSU: Shilole hataki vibabu, zake 'Serengeti Boy'

WIKI hii kunachimbika! Ndivyo waumini wa mitandao ya kijamii wanavyosema baada ya kujikuta wapo katikati ya vichambo vya wanawake wawili mastaa, Mambi Kimambi na Shilole.

Mashabiki hao ambao walionekana kuvutana kila upande ukimtetea yule wanayemkubali, baada ya Mange kuanzisha kitimutim kwa 'kumchamba' Shilole tabia yake ya kuishi na wanaume wenye umri mdogo.

"Hivi Shilole my dear, hivi kwani ni lazima uolewe jamani unanisikitisha utatumika na hivi vitoto mpaka lini, hizo hela za kuwalea hao vijana wenye mama zao si uwawekee wanao 'savings bank' jamani, hivi Bongo ndiyo tuseme wanaume hakuna kabisa, mwanamke mzuri mwenye shughuli zake kama Shilole anakosa kabisa mwanaume wa maana hadi inabidi alee kimtu ili akiite mume". Alianza Mange.

Kisha Shilole akaja juu akisema"Kuna muda ukifika pesa si kila kitu ila furaha ya mtu binafsi huja mbele, mimi ni muumini mkubwa wa hiyo falsafa, tatizo la wanawake wengi bado wapo katika desturi ya kuchuna ili waendelee kwa kutengemea vibabu dhambi hiyo iniepuke,"

Kisha akapigilia msumari "Penzi la kudandia ama kushea na mababa au vibabu vilivyooa siwezi sio vitu vyangu 'and besides Romy ni above 30' tena mwenye shughuli zake kiuchumi... yeye sio hivyo mnavyomtafsiri, samahani dada yangu hayakuhusu." Baada ya vichambo hivyo, mashabiki nao wakajikuta wakiraruana kwa maneno kwa kila mmoja akieleza maoni yake tofauti.

## Usiteme 'big G' kwa karanga za kuonjeshwa

**Na Adam Fungamwango**

KATIKA maisha kuna mambo mengi sana ya kushangaza na ya kusikitisha. Na kuna watu hujifunza kutokana na makosa ya watu wengine.

Hapa ulimwenguni mtu anaweza kuwa na kitu mkononi, lakini asikione cha thamani hadi pale atakapokipoteza, kupotea au kunyang'anywa.

Ndiyo maana waswahili wakaja wa misemo mingi, kama vile 'mbuzi hajui thamani ya mkia wake hadi ukatwe'. Kutunza kitu ulichonacho, au kukishikilia kisikuponyoke, tunafundishwa na filamu hii iitwayo 'Fau'.

Imechezwa na mzee Muhogo Mchungu, Madebe Lidai, Moza Abdallah, Lameck Kae, na wengineo.

Mussa anaishi vema na mkewe na mtoto wake Kidawa. Lakini Mussa mambo yanakuwa mengi. Huyu jamaa ni kama Athumani, hapishi chambo.

Siri ni ya mmoja, hakuna siri ya watu wawili. Mkewe Mussa mama Kidawa anatambua kuwa mumewe si mwaminifu. Hakuliki wala hakulaliki, hadi Mussa akatoa talaka moja. Mke kiguu na njia kwao.

Huku nyuma baada ya muda mrefu, wazazi wanachoshwa na tabia ya kijana wao Mussa, hivyo wanamwambia ama amrudie mkewe, au aondoke pale nyumbani na mtoto wake, kwani amechoka kumtunza mtoto ambaye ana baba na mama.

Mussa anafanya kazi kwenye duka la Madebe Lidai. Lakini ana mpenzi wake mmoja anaitwa Fau. Huyu ni mtoto wa mjini. Ni binti anayejua ya usiku na ya mchana.

Anachofanya anamchuna tu mtoto wa watu, halafu anachohitaji hapati, badala yake ahadi tele. Wazazi wanamkalisha chini Mussa na kumwambia amrudie mkewe ili walee mtoto, badala ya kupuyanga huku na huku. Mussa mwenyewe hasikii wala haambiwi kwa Fau, japo hajaionja hata asali yenyewe.

Mwenyewe anawaambia wazazi wake kuwa si lazima kumrudia mkewe, badala yake ataleta mwanamke mwingine. Mama yake anakwenda hadi kwa mama Kidawa kumuomba arejeane na kijana wake, lakini mama Kidawa anakataa katakata.

Chovya chovya, humaliza buyu la asali. Pesa alikuwa Mussa anamhonga Fau kutoka kwenye duka la tajiri yake, linasababisha duka hilo kuanza kufilisika.

Madebe anaamua sasa kumsimamisha kazi Mussa kutokana na pesa kuwa hazionekani. Lakini tayari alishagundua tatizo. Baada ya kutimuliwa kazi, Mussa anakwenda kwa demu wake Fau na kumweleza kuwa ametimuliwa kazi, lakini asijali.

Fau alimfukuza kama hamjui. Mussa aliondoka na alipofika kwenye mti mmoja mkubwa akikaa chini na kuanza kulia. Ukiona mtu mzima analia ujue kuna jambo.







## Weusi wa Official Nini burudani tosha

MSANII wa muziki wa Bongo Fleva, Official Nini, amesema ngozi yake ya asili na jinsi anavyojiweka ni kitu pekee wanachokipenda mashabiki wake.

Hata hivyo, amesema hakuna kitu anachokifanya akiwa na Nay wa Mitego, licha ya kuposti picha akionekana na bosi huyo wa lebo ya Free Nation, ambayo inammiliki kwa sasa.

"Ile picha ilikuwa ni ya muda mrefu nilijisikia tu kumchokoza wifi, mimi sina mke mwenzangu maana naogopa nisije nikaharibu ndoa za watu, yule wa sasa hivi ni wifi yangu kwa boss wangu siku nikikutana naye nitamwambia ampende sana boss wangu, hicho ndicho kikubw," amesema Nini.



WALIOTIKISA 2020

## Diamond, Kiba weka nikuweke

**Na Adam Fungamwango**

MIAKA itokako iendako hakujulikani. Mwaka 2020 umekwenda na hautorudi tena. Hakuna mwanadamu yeyote aliye hai, au atakayezaliwa baadaye atakayeushuhudia tena. Utabaki kwenye rekodi na historia milele na milele.

Ulikuwa na mengi mazuri, lakini kwenye ubaya, binadamu wote duniani wataukumbuka mwaka huu na kitu kimoja tu. Nacho ni ugonjwa wa COVID-19, unaosababisha na virusi vya corona. Mbali na vifo na watu kuugua, lakini ulibadilisha hata staili ya maisha ya binadamu.

Ingawa duniani bado upo, lakini si kwa nguvu ile ya mwanzo.

Leo tutaangalia wasanii wa kiume nchini Tanzania ambao wamefanya vizuri kwenye muziki na hata kukubalika na mashabiki wao kwa mwaka uliomalizika kwa 2020.

**DIAMOND PLATINUMZ**

Bado anaendelea kuwa kinara wa wasanii wote nchini Tanzania kwa kuwa na wafuasi wengi, kutoa ngoma zinazopendwa, lakini kutoka video zenye ubora wa hali ya juu, huku akifanya kazi na wasanii wengi tofauti Afrika kwa duniani kote.

Mfano mwishoni mwa mwaka huu, ametoa ngoma na mwanamuziki Koffi Olomide inaitwa 'Waah'. Shidhani kama inahitaji maelezo mengi juu ya msanii huyo maarufu.

**ALI KIBA**

Naye akaendelea kuwa msanii ambaye ana mvuto kwa mashabiki wengi nchini Tanzania. Japo amekuwa hatoi ngoma nyingi sana na hana makeke, lakini anaonekana ana ngome kubwa ya wafuasi, lakini ngoma anazotoa zimekuwa zikizidi kumpa heshima.

Siku chache tu zilizopita ametoa ngoma ya kufungia mwaka 2020 iitwayo 'Nakupenda' akimshirikisha Dj Sbu. Ngoma zingine zilizotikisha mwaka huu ni 'Mediocre', miezi mitatu iliyopita na 'Dodo' iliyotoka miezi minane iliyopita.

**HARMONIZE**

Kabla sijaenda mbali sana, jamaa huyo tayari ameshatoa ngoma yake ya kufungia mwaka 2020 aliyoiita 'Wapo'. Ni ngoma mpya ambayo tayari imekuwa na maneno mengi kuwa ni ya madongo.

Naye kwa sasa amekuwa msanii mwenye vishindo na mbwembwe nyingi. Mwezi mmoja uliopita ametoa ngoma aliyoiita 'Ushamba' na kwa siku za karibuni amekuwa akitoa ngoma mpya karibuni kila mwezi.

**MEJA KUNTA**

Kwa upande wa muziki wa singeli kwa mwaka 2020, haukuwa wa Sholo Mwamba, Man Fongo, Dula Makabila, Msaga Sumu, wala S Kide, bali Menja Kunta.

Huyu mwamba aliuteka kwa mwaka ulimalizika kwa ngoma zake kali ambazo pia zilikuwa zikiambatana na matukio, ambayo yalionyesha kabisa ni ya kupanga.

Mfano alivyosingizia amekufa akatoa ngoma 'Wanga Wabaya'. Zingine ni 'Chura Super Star, 'Naumia Moyo' na nyingine nyingi.

**MBOSSO**

Hakudhaniwa, lakini ukweli ndiyo huo. Msanii Mbosso amekuwa mmoja wa wasanii ambao wametisha msimu ulioisha, kutokana na aina yake ya nyimbo ambazo amekuwa akitoa.

Ngoma kama 'Fall', 'Sina Nyota', 'Tamba' na nyingine nyingi, zimemfanya kuwa mmoja wa wasanii bora kabisa mwaka 2020.

# Tyrese, Samantha wapeana talaka



MSANII wa filamu wa Marekani, Tyrese Gibson na mkewe Samantha, wameachana baada ya kuishi katika ndoa karibu miaka minne.

Nyota huyo kutoka Hollywood, ameandika katika ukurasa wake wa Instagram, kuwa wote wawili baada ya kufikiria na kuomba dua, wameamua kuvunja ndoa hiyo.

"Tumeamua kuweka taarifa hii inayouma na kurudisha nyuma maendeleo yetu. Baada ya kufikiri sana, kushirikiana na kuomba kwa bahati mbaya tumeamua kuivunja ndoa yetu kwa kupeana talaka," amesema Tyrese.



## Wenye ushawishi Nigeria 2020

MWAKA 2021 umeingia katika hali ya kufurahisha, lakini kwa wasanii 10 wa Nigeria wana furaha zaidi baada ya kutajwa kuwa wanaongoza kwa ushawishi nchini humo.

Kulingana na mtandao wa Pulse, mastaa hao wametajwa na wananchi kuwa wana wafuasi wengi kutokana na ushawishi wao kwa mwaka 2020.

Wasanii waliotajwa ni Laycon, Olamilekan Moshood Agbeleshe, maarufu kama Erica ambao wote washiriki wa Big Brother Naija, wanamuziki Falz, Wizkid, Davido, Burna Boy, Don Jazzy, mchekeshaji Mr Macaroni na Josh 2 Funny.

## Panchy hawakubali Wanigeria

MWIGIZAJI wa filamu kutoka Cameroon, Panchy CY, amewataka raia wa nchi hiyo kutowakubali wasanii wa muziki wa Nigeria, wanaokwenda huko kutoa burudani.

Kulingana na nyota huyo anayeheshimika nchini humo, alisema yeye aliishi Nigeria, alishuhudia vitendo vya kubaguliwa na kutengwa.

Amesema Nigeria wageni wanaishi kwa kushambuliwa na ni lazima Wacameroon nao kuwabania wasanii kutoka nchi hiyo.





## Hawa kiboko kwa mapozi 2020

Katika maisha ya mastaa moja ya sifa ambazo wanapenda kuwa nazo ni kuwa na m mwonekano mzuri.

Kulingana na mtandao wa Pulse, wasanii watano wa Nigeria wameongoza kuwa na mwonekano mzuri kwa mwaka 2020.

Waliongia katika orodha hiyo ni mwanamitandao ya kijamii, Ebuka Obi-Uchendu, Neo wa Big Brother Naija, mwigizaji Etim Effiong, Falz ambaye ni mwandishi wa habari na mwanamuziki Paul Okoye.

## Big Lo hatunaye tena

MWANAMUZIKI wa Hip hop kutoka Nigeria, Lotanna Udezue, maarufu kama Big Lo amefariki dunia baada ya kupata matatizo ya figo kwa muda mrefu.

Kifo cha msanii huyo kimetangazwa na mwanamuziki mwenzake Jazzman Olofin, kupitia ukurasa wake wa Instagram.

"Mpendwa BIGLO, tuna habari yake ya huzuni kuwa amefariki dunia. Alipigana kwa kila njia, lakini Mungu amempenda zaidi," ameandika Jazzman.



MAKALA

# DUNIA ILIVYOUPOKEA 2021

**Na Mwandishi Wetu**

SHEREHE za kuingia mwaka mpya kwa kawaida zinakuwa na mbwembwe za kila aina, lakini mwaka huu nchi nyingi duniani zimeweka vizuizi na kutibua shamrashamra hizo.

Kwa mfano katika nchi hizo zilizoweka vikwazo vikali kwa ajili ya kupambana na virusi vya corona, watu hawakuweza kuona mikusanyiko barabarani na viwanja vikubwa kwa ajili ya kushuhudia kurushwa kwa mafataki yenye kutoa rangi za kupendeza.

Maonyesho ya mafataki yaliyokuwa yakishuhudiwa kuanzia Jiji la New York, Marekani hadi Sydney, Australia yalipigwa marufuku.

Hakukuwa na sherehe katika mabara ya Ulaya, Marekani ya Kusini na Kaskazini na hata Asia, kwa kuhofia kusambaa aina mpya ya ugonjwa wa Covid-19 ambao inaelezwa unasambaa kwa kasi kubwa.

Nchini Ufaransa, zaidi ya polisi 100,000 waliwekwa mitaani kushika doria katika barabara ili kuhakikisha amri ya kutotoka nje nyakati za usiku zinatekelezwa.

Zaidi ya watu milioni 1.8 wamefariki kutokana na ugonjwa wa corona tangu janga hilo lilipoanza mwaka 2019. Zaidi ya watu milioni 81 wameripotiwa kuambukizwa.



Mafataki yakirushwa angani katika Jiji la Sydeney nchini Australia bila kushuhudiwa na umati wa watu kama ilivyokuwa kawaida yake wakati wa sherehe za mwaka mpya.

## •Corona yatibua vionjo na shamrashamra

**NINI KILIFANYIKA?**

Nchini Ufaransa, serikali iliamuru uwepo wa usalama katika maeneo ya mijini kuanzia saa 2:00 usiku ya Alhamisi, wakati amri ya kutotoka nje ilipoanza.

Ufaransa imeweka amri hiyo ya kutotoka nje huku mabaa, na kuruhusu migahawa na maeneo ya vivutio vya watu kubaki wazi wakati wa kukaribisha mwaka mpya.

Katika hotuba yake ya mwaka mpya, Rais Emmanuel Macron, amewaaonya wakosoaji wake wanaolalamikia kujikokota kwa mpango wa kutoa chanjo, na kuapa kushughulikia suala hilo katika muda unaostahili.

Upande wa Uingereza ambako virusi vipya vya corona vinavyosambaa kwa kasi vimegunduliwa watu wamelazimika kubaki ndani ya nyumba zao wakati mwaka mpya ukiwadia.

Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson, ametoa wito wa watu kuzingatia masharti yaliyowekwa.

Barabara za mji wa London zilikuwa kimya wakati wa mkesha wa mwaka mpya baada ya polisi kuomba watu washerehekee majumbani mwao.

Badala ya sherehe za kawaida zinazojumuisha mikusanyiko ya watu, onyesho la fataki lilifanywa katika maeneo tofauti ya jijini humo.

Huko nchini Ireland, vikwazo zaidi viliongezwa kuanzia Alhamisi, kwa kupiga marufuku watu kutembeleana majumbani na kufunga maduka ambayo hayauzi bidhaa muhimu na kudhibiti usafiri wa hadi kilomita tano.

Nchini Ujerumani imeweka amri ya kutotoka nje hadi Januari 10. Serikali imepiga marufuku uuzaji wa fataki na kuweka vikwazo vikali vya kudhibiti idadi ya watu wanaokusanyika pamoja.

Katika hotuba yake ya mwaka mpya inayotazamiwa kuwa ya mwisho kwake kama kiongozi wa Ujerumani, Angela Merkel, alikemea watu wanaopotosha umma kuhusiana na janga hilo.

Amesema anashangazwa na jinsi uwongo na ukatili unavyotumiwa na watu bila kujali hisia za wale waliyopoteza wapendwa wao kutokana na ugonjwa wa corona

Italia, amri ya kutotoka nje iliwekwa kuanzia saa 4: 00 usiku, huku baa, migahawa na maduka yakifungwa.

Hata hivyo, Kiongozi wa Katoliki Duniani, Papa Francis, ameshindwa kuongoza ibada ya mwaka mpya mjini Rome badala ya kupata maumivu ya nyonga sugu.

Amri ya kutotoka nje kwa raia imewekwa pia katika nchi za Uturuki na Uholanzi.

**MAREKANI HALI IKOJE?**

Maofisa wa serikali wameweka vikwazo vya kudhibiti sherehe za mwaka mpya katika majimbo mengi na miji ya nchi hiyo.

Mjini New York, mnara mpira wa raba wa taa uliwashwa wakati wa kuvuka mwaka, lakini eneo hilo halikuwa na watu.

Kikundi kidogo cha wafanyakazi wa kutoa huduma za afya, ambao wanajulikana kama "shujaa wa 2020", na familia zao waliruhusiwa kuingia kama wageni maalum katika maeneo yaliyotengwa.

Fataki zilipigwa marufuku katika miji mbalimbali ikiwamo San Francisco na Las Vegas.

Katika hotuba yake ya mwaka mpya iliyowekwa kwenye Twitter, Rais wa Marekani, Donald Trump, amewapongeza watengenezaji wa chanjo na kuita kama miujiza ya kimatibabu.

Pia amepongeza juhudi wafanyakazi wa 'Operation Warp Speed', mpango wa Marekani unaolenga kutengeneza na kuwasilisha chanjo kwa juhudi zao.

Lakini hakuwataja wala kutoa rambirambi kwa Wamarekani wanaofikia 350,000 waliofariki kutokana na corona.

**NCHI ZA ASIA-PASIFIKI**

Nchi inayoongoza kwa mapokezi mazuri inapoingia mwaka mpya ni Australia. Hata hivyo, maonyesho ya fataki ya Sydney yalifanywa kama kawaida, lakini watu hawakuruhusiwa kukusanyika kujionea kama ilivyo ada.

"Hatutaki kuwa na hafla ambayo itasambaza virusi katika mkesha wa mwaka mpya," Waziri Mkuu wa New South Wales, Gladys Berejiklian, alisema.

Wakazi wengi wa Sydney walifuatilia onyesho hilo kwenye televisheni zao nyumbani, ambako watu watano tu waliruhusiwa kuwa pamoja.

Huko nchini China, tamasha la mwangaza linalofanyika kila mwaka katika mji mkuu wa Beijing lilifutiliwa.

Jambo la kushangaza katika mji wa Wuhan, ambako inadhaniwa kuwa chimbuko la janga la corona, maelfu ya watu walikusanyika katikati ya mji huo kusherehekea huku maputo yakiachiliwa kupaa angani.

Japan ilifuta sherehe za jadi za kukaribisha mwaka mpya ambayo Mfalme wa nchi hiyo, Naruhito na familia yake ilikuwa iwasalimie watu.

Nchini India, Jiji la Delhi na miji mingine kadhaa, amri ya kutotoka nje usiku na masharti mengine ya kuzuia mikusanyiko mikubwa ya watu wakati wa mwaka mpya iliwekwa.

Hata hivyo nchini New Zealand, ambako amri kali ya kutotoka nje na kufungwa kwa mipaka iliwekwa na kusaidia kuangamiza ugonjwa huo, sherehe za kuukaribisha mwaka mpya ziliandaliwa kama kawaida.

**Kwa msaada wa BBC**



Mnara wa mpira wa taa ulioko jijini New York nchini Marekani, ukiwaka bila ya kushuhudiwa na watu katika mkesha wa mwaka mpya wa 2021.

MAKALA

# UCHAGUZI WA UGANDA

## •Museveni na uhai wa Afrika Mashariki

Na Mwandishi Wetu

UGANDA inajiandaa kufanya uchaguzi wake mkuu Januari 14, mwaka huu, jumla ya wagombea 11 wamejitokeza kuwania nafasi ya urais ambayo inaendelea kukaliwa na Mzee Yoweri Kaguta Museveni (pichani).

Museveni anaingia katika orodha ya viongozi wachache walio madarakani barani Afrika ambao wanaweza kujisifu wanatokana na vuguvugu la Pan Africanism.

Hata hivyo, wakati raia wa Uganda wanajiandaa kushiriki zoezi la upigaji kura kuchagua viongozi wao wa ngazi mbalimbali, swali la kujiuliza ni kwa nini uchaguzi huo ni muhimu kwa mataifa mengine yanayounda Jumuiya ya Afrika Mashariki?



**NDOTO YA TAIFA MOJA**

Kulingana na Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC), hakuna siri kwamba mmoja wa viongozi ambao wamekuwa wakizungumzia kuhusu umuhimu wa Shirikisho la Afrika Mashariki ni Yoweri Museveni.

Ndoto ya kuona Afrika Mashariki inakuwa taifa moja lenye nguvu za kiuchumi na kijeshi ni kiongozi huyu ambaye amedumu kwa miaka 36 sasa.

Museveni anaamini kwamba Afrika ilitawaliwa kirahisi na wakoloni na inaendelea kunyonywa hadi sasa kwa sababu ya kukosa umoja. Jambo moja ambalo amekuwa akilipigania mara kwa mara ni kuundwa kwa Shirikisho hilo la kisiasa.

Kwa hali ilivyo sasa, hamu kubwa ya shirikisho hilo iko zaidi kwa Museveni kuliko kwa viongozi wengine kwa sababu tofauti.

Kimsingi, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, EAC inapita katika kipindi kigumu kwa sababu ya siasa za kikanda na kidunia ambazo sasa zinaangalia ndani ya nchi zaidi kuliko nje.

Shirikisho la Afrika Mashariki litaimarisha soko kubwa la bidhaa kwa wananchi wa eneo hilo. Hii itakuwa na mzunguko mkubwa wa mitaji na utaalamu, uimara wa ulinzi na usalama na uhusiano imara baina ya nchi hizo.

Falsafa hiyo ya Museveni ndiyo iliomfanya akubali Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Uganda (UPDF) likafanye kazi za kulinda amani katika nchi kama Somalia na kwingineko.

Ushindi wa Museveni utamaanisha Uganda, itaendelea kuwa mojawapo ya nchi inayoamini katika mambo ya kimajumuiya kwa ukanda na bara zima la Afrika.

**BOMBA LA MAFUTA**

Septemba mwaka jana, Tanzania na Uganda ziliingia katika makubaliano ya ujenzi wa bomba la mafuta litakalotoka Hoima hadi Bandari ya Tanga.

Bomba hilo litakuwa na urefu wa kilomita 1,445, huku mradi mzima ukigharimu zaidi ya dola bilioni 3.5 za Marekani.

Kenya ilikuwa ikiutaka mradi huu, Tanzania ilifanikiwa kuupata kutokana na mahaba ambayo Museveni anayo kwa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere.

Museveni alianza kujipambanua kama mwanasiasa na mwanaharakati katika miaka ya 1960, wakati akiwa mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM). Aliishi Tanzania na kuingia kwake madarakani kuliko na msaada wa majeshi ya nchi hiyo.

Mradi huu wa bomba la mafuta ni mkubwa zaidi katika Afrika, unatarajiwa kuwa na faida za kiuchumi kwa nchi hizo mbili.

Hata hivyo, ni vigumu kufahamu kama kiongozi mpya wa Uganda kama akichaguliwa ataendelea na mkakati huo na Tanzania.

Kwa sababu hiyo, kama Museveni ataendelea kuwa madarakani, mradi huo mkubwa unatarajiwa kubaki kama ulivyo na kunufaisha raia wa nchi hizo mbili.

**DEMOKRASIA**

Endapo Museveni atashinda katika uchaguzi huu, atakuwa amefikisha miaka 40 akiwa madarakani wakati atakapomaliza muda wake wa miaka mitano.

Atakuwa na rekodi mpya ya kuwa kiongozi aliyedumu madarakani kwa muda mrefu zaidi katika Afrika Mashariki.Kama akichaguliwa tena itakuwa ni pigo kwa wale wanaoamini kuwa demokrasia ni viongozi kukaa madarakani kwa vipindi maalumu.

Hata hivyo, ushindi wa Museveni, utatuma ujumbe kwa nchi wanachama wa EAC na nchi nyingine za Afrika kuwa hakuna tatizo kubadili katiba na kuendelea kukaa madarakani.

**WAPINZANI WAKE**

Mpinzani wake mkubwa, mwanamuziki Bobi Wine, anapitia wakati mgumu katika kampeni zake.

Yeye na wafuasi wake kila mara anakumbana na vipigo na msururu wa kesi. Hata hivyo, ameahidi kukabiliana na hali hiyo ili kuwapatia nafasi wananchi kutoa majibu yao kwa kupitia sanduku la kura.

Hakuna anayempa nafasi kushinda katika uchaguzi huu kwa sababu ya uwezo wa kirasilimali, kimtandao na mbinu za kiuchaguzi za chama tawala cha NRM ni mkubwa.

**NGUVU YA VIJANA**

Uganda ni mojawapo ya mataifa yenye watu wengi wenye umri mdogo. Kulingana na takwimu rasmi za serikali, umri wa wastani wa Waganda ni miaka 16.

Mgombea urais kupitia upinzani, Bobi Wine, ana umri wa miaka 38, ambao kwa nchi kama Tanzania, asingeruhusiwa kuwania nafasi hiyo kutokana na katiba inataka mtu afikishe miaka 40. Endapo Bobi atashinda basi ni wazi atatoa mwamko kwa vijana wa Afrika kuingia katika siasa na kuwania nafasi za juu za kisiasa.

Uchaguzi wa Uganda utakuwa unafuatiliwa na vijana wengi barani Afrika si kwa sababu Bobi ni kijana mwenzao wanayemfahamu, lakini kwa sababu ushindi wake unaweza kufungua fursa mpya.

## HABARI KIMATAIFA

## Walinda amani Darfur wakamilisha kazi

**KHATOM,** Sudan

UMOJA wa Mataifa(UN) na Umoja wa Afrika (AU), zimekamilisha kazi ya kulinda amani katika Jimbo la Darfur nchini Sudan.

Vikosi vilivyopewa kazi ya kulinda amani vimefikia mwisho wa majukumu yao baada ya kuwepo katika eneo hilo lililokumbwa na migogoro kwa muda wa miaka 13.

Umoja wa Mataifa ulisema hatua hiyo inatekeleza azimio la Baraza la Usalama lililofikiwa Desemba 22, mwaka jana. Kufikia ukomo wa vikosi vya Umoja wa Mataifa (UNAMID), kunatoa nafasi jukumu la ulinzi wa raia kuhamishiwa kwa serikali ya Sudan.

Hata hivyo wanaharakati wa kutetea haki za binadamu wameikosoa hatua hiyo, wakisema hali ya usalama bado ni ya wasiwasi katika Jimbo la Darfur.

Zoezi la kuondoka askari hao wa wapatao 16,000, linatarajiwa kukamilika Juni 30 mwaka huu.

Msemaji wa UNAMID, Ashraf Eissa, alisema ujumbe wa kisiasa wa Umoja wa Mataifa utakaosaidia kipindi cha mpito nchini Sudan, utawekwa katika Jimbo la Darfur baada ya UNAMID kuondoka. **DW**

# Uingereza yaaga rasmi EU usiku wa Mwaka Mpya

**LONDON,** Uingereza

UINGEREZA imeachana rasmi na mkataba wa Umoja wa Ulaya (EU) wa Brexit usiku wa saa 6: 00 kuingia Januari mosi 2021, na kuanza utekelezaji mpya wa mpango wa kiuchumi na umoja huo.

Mpango mpya ambao umeanza utekelezaji ni ule unaohusu usafiri, biashara, uhamiaji na ushirikiano wa kiusalama kuanza kutekelezwa.

Waziri Mkuu wa nchi hiyo, Boris Johnson, alisema Uingereza ina uhuru mikononi mwake na uwezo wa kufanya kila kitu tofauti na bora, sasa muda uliokuwa ukisubiriwa umekwisha.

Uingereza ilijiondoa katika muungano huo wa kisiasa na kiuchumi uliyo na nchi wanachama 27 miaka mitatu na nusu iliyopita, baada ya raia wa Uingereza kupiga kura ya maoni mwaka 2016.

Lakini iliendelea kufuata sheria za kibiashara za EU katika kipindi cha miezi 11, wakati pande hizo mbili zikishauriana kuhusu ushirikiano wao wa kibiashara wa siku zijazo.

Baada ya mazungumzo hayo kukamilika, mkataba wa kihistoria uliafikiwa katika mkesha wa Krismasi. Ulikuwa sheria kamili Jumatano baada ya kuidhinishwa na bunge.

**Waziri Johnson ambaye alikuwa kiungo muhimu katika kampeni ya Brexit katika kura ya maoni ya mwaka 2016, alisema ulikuwa wakati wa maajabu kwa Uingereza.**

Chini ya sheria hilo mpya, iliyoanza kutekelezwa saa 6:00, wafanyabiashara wa Uingereza watafikia masoko ya ndani ya EU bila kulipishwa kodi, ikimaanisha bidhaa zinazosafirishwa kati ya Uingereza na Ulaya hazitatozwa kodi.

Lakini inatakiwa nyaraka zaidi kwa wafanyabiashara na watu wanaosafiri kwenda nchi za EU. Hata hivyo bado kuna wasiwasi kuhusu nini kitatokea kwa benki na watoaji huduma, ambazo ni sehemu kuu ya uchumi wa Uingereza.

Kunatarajiwa kuwapo na msongamano katika kituo cha Dover siku ya kwanza ya mwaka huu, wakati uangalizi wa mpakani utaanza kutekelezwa.

Waziri Johnson ambaye alikuwa kiungo muhimu katika kampeni ya Brexit katika kura ya maoni ya mwaka 2016, alisema ulikuwa wakati wa maajabu kwa Uingereza.

Katika ujumbe wake wa mwaka mpya, alisema Uingereza sasa iko huru kufanya vitu tofauti, na ikiwezekana vyema zaidi kuliko marafiki zao wa Ulaya.

"Uhuru wetu uko mikononi mwetu, tunaweza kuamua tutakacho," alisema.

Lord Frost, ambaye ni mshauri mkuu wa Ungereza, aliandika kwenye Twitter kuwa Uingereza imekuwa huru tena huku mbunge mkongwe wa Conservative, Sir Bill Cash, akisema matokeo yalikuwa ni ushindi kwa demokrasia.

Hata hivyo, Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron, alisema Uingereza itasalia kuwa rafiki na mshirika mwaminifu.

Waziri wa Mambo ya Nje wa nchi hiyo, Simon Coveney, alisema sio jambo la kusherehekea na uhusiano wa Uingereza na Ireland utakuwa tofauti kuanzia wakati huo, lakini aliwatakia kila la heri.

Wanaopinga kujiondoa Brexit, walisema hatua hiyo itashuhudia nchi hiyo ikifanya vibaya zaidi kuliko wakati ilipokuwa ndani ya EU.

Waziri wa kwanza wa Uskochi, Nicola Sturgeon, ambaye alama yake ni kuirejesha Uscochi EU, aliandika kwenye mtandao wa Twitter.

"Uscochi itarejea hivi karibuni, Ulaya. Endelea kuangaza."

Makao makuu ya Ulaya, Brussels, ilikuwa katika hali ya utulivu baada ya mchakato wa Brexit kukamilika, lakini kuna hali ya kutoridhika kwa baadhi ya wanachama. **BBC**



Mkusanyiko wa watu wakifurahia mwaka mpya 2021 katika bwawa la maji la umma maarufu kama Golden Mile, katika mji wa Durban nchini Afrika Kusini jana.
**PICHA: THE TIMES**

# Watu 25 wauawa na waasi DRC

**KIVU,** Kongo-DRC

WATU 25 wameuawa Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, katika mashambulizi ambayo inadaiwa kufanywa na kundi la waasi la ADF.

Mkuu wa Wilaya ya Beni, mkoani Kivu Kaskazini, Donat Kibuana, aliliambia shirika la habari la AFP, kuwa jeshi la serikali ya Kongo liliwafukuza waasi hao.

Miili ya watu hao waliouawa ilisambaa eneo hilo baada ya waasi hao kuwavamia wakiwa mashambani mwao na kuwaua kwa risasi.

Mauaji hayo yalitokea katika kijiji cha Tingwe, kilichoko umbali wa kilomita nane kutoka mji wa Eringeti. Kiongozi wa asasi za kiraia katika kijiji hicho, Bravo Mohindo, alisema idadi ya waliouawa sio chini ya watu 30.

"Watu hao walikwenda kwenye mashamba yao kujiandaa na mkesha wa sikukuu ya mwaka mpya, ADF waliwashambulia mmoja baada ya mwingine," alisema Vukulu. Aliongeza "Tulikuwa tumeliarifu jeshi la serikali kuwa waasi hao wamepita katika eneo hilo, wakitokea kaskazini mashariki mwa kuelekea kaskazini mashariki mwa mji wa Eringeti, lakini jeshi hilo halikuchukua hatua haraka." **DW**

# Serikali kuwawezesha vijana wabunifu TEHAMA

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile, amesema serikali itaweka mazingira wezeshi ya kuendeleza vijana wabunifu wa teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA).

Dk. Ndugulile aliyasema hayo jana wakati wa ziara yake katika Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) na Ndaki ya TEHAMA ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (COICT).

Alisema vijana wanabuni mifumo mbalimbali ya TEHAMA ya kutatua changamoto za wananchi, lakini wanakosa mazingira wezeshi ya kuendeleza na kukuza ubunifu wao kama vile kupatiwa muda maalumu wa kuingiza sokoni kwa kufanya majaribio na kukubalika kwa wananchi bila kulipia gharama za usajili, kupata masoko, malipo ya kodi na leseni kuendana na matakwa ya uendeshaji wa kampuni na biashara nchini.

Alisisitiza kuwa azma ya serikali ni kuendeleza wabunifu wa TEHAMA, ili kutengeneza mifumo kuendana na mahitaji ya wananchi badala ya kuendelea kununua mifumo hiyo kwa gharama kubwa kutoka nje ya nchi huku serikali ikitumia fedha nyingi kununua mifumo hiyo.

Waziri alisema utengenezaji wa mifumo ya TEHAMA nchini utaongeza wigo wa matumizi ya intaneti na huduma za mawasiliano na itajibu changamoto za wananchi.

Alitoa rai kwa Watanzania kujenga imani ya kutumia teknolojia rahisi zinazobuniwa na vijana wa ndani ya nchi bila kujali umri, uzoefu au majina ya kampuni zao.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa COSTECH, Dk. Amos Nungu, alisema vijana wameanzisha zaidi ya kampuni 20 za mifumo ya TEHAMA na tayari mifumo hiyo inasaidia kukusanya kodi kwenye halmashauri, kuwawezesha vijana kusoma VETA kwa njia ya mtandao na TIGO kuhifadhi taarifa za wateja wake.

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu, Utafiti na Ubunifu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Prof. Benadetha Kiliani, na Mkuu wa Ndaki ya TEHAMA ya Chuo hicho, Dk. Mussa Kisaka, walisema wako tayari kushirikiana na wizara ili kuendeleza vijana wabunifu na watafiti wa TEHAMA nchini.

Akizungumza kwa niaba ya vijana wabunifu wa TEHAMA, Geofrey Magila, aliiomba serikali kuwawezesha wakubalike na kuaminika na wapewe kazi badala ya kampuni zao kufanya kazi kwa kutumia mgongo na majina ya kampuni zingine kwa kuwa kampuni zao ni changa na hazina mtaji wa kutosha kuingia kwenye ushindani wa zabuni zinazotangazwa.

"Tulipata kazi kutoka kampuni ya AIS ya simu za mkononi ya Malyasia yenye wateja zaidi ya milioni 50 ambao walituamini na tuliwatengenezea mifumo ya kulinda taarifa za wateja wao, ndipo baadaye baadhi ya kampuni za ndani ya nchi zikaanza kutuamini," alisema Magila.



Mke wa marehemu Yusufu Deus akiwa na waombolezaji waliofika kwenye la Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania –KKKT kwa ibada ya kuaga mwili wa mfanyabiashara wa chipsi eneo la Makumbusho jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Mbunge amtoa hofu RC ujenzi madarasa

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MBUNGE wa Mafia, Kipanga Juma, amemwahidi Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Evarist Ndikilo, kuwa yeye na viongozi wengine watahakikisha wanafunzi waliofaulu kuingia kidato cha kwanza wanaanza shule mwezi huu.

Kipanga ambaye ni Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, alisema watakaa na viongozi wa wilaya ya Mafia kusimamia ujenzi wa vyumba vitakavyotosheleza wanafunzi wote wa wilaya hiyo, ambao wanatakiwa kujiunga na kidato cha kwanza mwezi huu.

Kipanga aliyasema hayo juzi katika Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa wa Pwani, ambayo pamoja na mambo mengine, ilijadili suala la watoto waliofaulu, lakini hawakupangiwa shule.

Hali ya ufaulu katika Wilaya ya Mafia ni asilimia 89.94, ambapo wanafunzi 1,153 wanatakiwa kuanza masomo ya kidato cha kwanza huku vyumba vinane vya madarasa vikihitajika.

Wanafunzi 30,212 waliohitimu darasa la saba mwaka jana, walifaulu kwa daraja A-C na inaelezwa kuwa ufaulu wa mwaka jana ulipanda kufikia asilimia 86.9 kulinganisha na mwaka 2019 ambapo ilikuwa asilimia 85.13.

## Diwani abainisha dira ya maendeleo

**Na Maulid Mmbaga**

DIWANI wa Ilala, Saady Khimji, ametoa dira ya maendeleo katika eneo hilo na kueleza mpango wa serikali kujenga zahanati na kuboresha huduma za afya katika kata hiyo.

Aliyasema hayo, juzi, katika kikao kilichofanyika ndani ya kata hiyo na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wakiwamo wenyeviti wa mitaa, watendaji na maofisa wa polisi.

Khimji alisema viko vipaumbele mbalimbali katika kipindi cha uongozi wake ambavyo ni pamoja na ukarabati na ujenzi wa madarasa mapya, lakini matazamio ni kupata shule ya kidato cha tano na sita.

Kwa upande wa miundombinu, alisema mpango wa serikali ni kuboresha barabara zote za mitaani pamoja na kuzijenga kwa kiwango cha lami kilomita tano.

Pia alisema serikali ina mpango wa kujenga soko jipya la kisasa na kuboresha soko la sasa.

"Kero kubwa ni suala la takataka, kupitia mkandarasi wa kukusanya taka serikali imejipanga kuondoa kero hiyo na tunawaomba wananchi watoe ushirikiano hasa kwa kulipa ada ya taka," alisema.

# Madiwani wapewa kibarua ujenzi madarasa

**Na Steven William, TANGA**

MKUU wa Mkoa wa Tanga, Martine Shigela, amezidi kuwasisitizia madiwani wa halmashauri zote mkoani hapa kwenda katika kata zao kuanzisha ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule za msingi na sekondari pamoja na kutengeneza madawati ya kukaa wanafunzi.

Shigela alitoa agizo hilo juzi wilayani Muheza wakati akizungumza na watumishi na madiwani wa halmashauri ya Wilaya ya Muheza kuhusiana na ujenzi wa madarasa na mambo mengine.

Pamoja na kuwapongeza madiwani hao kwa kuchaguliwa na wananchi katika kata zao, alisema sasa wanapaswa kusimamia miradi ya maendeleo na kusikiliza kero za wananchi.

Aliwataka madiwani hao kwenda kuwahamasisha wananchi na wadau mbalimbali wa maendeleo kujitolea nguvu zao kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule za msingi na sekondari na serikali itasaidia ujenzi huo.

Shigela alisema hataki kusikia hata mtoto mmoja kuwa ameshindwa kwenda shuleni kutokana na upungufu wa vyumba vya madarasa au madawati, hivyo lazima madiwani wasimamie hilo kikamilifu.

Kwa mujibu wa Shigela, madiwani hawana budi kuwa makini katika kusimamia maendeleo katika kata zao ikiwamo ujenzi wa madarasa, ili watoto wasome wasirudi nyumbani hata mmoja.

Alisema shule zinafunguliwa hivi karibuni, hivyo lazima madiwani wajipange kwa kufahamu kunahitajika ujenzi wa vyumba vya madarasa na kutengeneza madawati ya kukaa wanafunzi.

Mkuu huyo wa mkoa alisema wanafunzi wanaojiunga na elimu ya msingi mwaka huu wameongezeka, hvyo vyumba vya madarasa kuwa vichache na madawati sasa inahitajika msukumo wa nguvu kupata vitu hivyo.

Kwa upande wa shule za sekondari, alisema wanafunzi wanaoanza kidato cha kwanza ni wengi, hivyo kunahitajika madawati katika shule zote za mkoa wa Tanga na kwamba hataki kusikia mwanafunzi amerudi nyumbani kwa sababu ya kukosa dawati.

# HADITHI

MAUAJI ya kutisha yanatokea ndani ya gesti moja maeneo ya Kigogo jijini Dar es Salaam. Mfanyabiashara Burhan anauawa ndani ya gesti ya Tukutane, akiwa na msichana mmoja mrembo aitwaye Mwanaidi. Polisi wanawakamata watu wote waliokutwa humo, pamoja na wafanyakazi wa gesti hiyo kwa ajili ya mahojiano. Lakini inaonekana muda ambao walikuwapo wapenzi hao hakukuwa na mteja mwingine yeyote zaidi yao.

Baada ya mahojiano ya kina, inaonekana kabisa kuwa Mwanaidi ndiyo muuaji. Je, ni kweli? Kwa nini alimuua mpenzi wake wakiwa wamejifungia chumbani? Fuatilia hadithi hii kwa makini ambayo mbali na kukutia simanzi, furaha na kukuburudisha, pia itakufundisha, elimu na kufunulia mambo ambayo hukupata kuyafikiria kabla.

# Lazima Apatikane - 2

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**

INSPEKTA Msiya wa Polisi Makao Makuu, ndiye aliyepewa kusimamia jalada kwa ajili ya upelelezi na kuchukua maelezo ya mtuhumiwa kabla ya kulipeleka mahakamani.

Mwanaidi alikaa kituoni kwa wiki moja, kwanza ikiwa akili yake ikae sawa kutokana na sakata lenyewe jinsi lilivyo kwani alikuwa amezirai kwenye tukio hilo, lakini ni kutaka kuchukua maelezo yenye kina na yenye uhalisia na si ya kudhani kwa sababu ilikuwa ni kesi nzito ya mauaji.

"Ni kweli ulikuwa unampenda Burhan?"

"Ndiyo afande."

"Kwa nini?"

"Kwanza alionekana kunipenda sana. Lakini alikuwa ananijali na kunipa pesa kwa kiasi ninachohitaji, kiasi kwamba nimeweza hata kumtumia mama Singida akanunua kiwanja na kama ningeendelea naye nina imani ningejenga."

Aliinua simu na kumuita Koplo Hamisi. "Mchukue mpeleke kwenye kile chumba halafu urudi hapa."

Dakika tano baadaye Koplo Hamisi alirejea kwa bosi wake Inspekta Msiya.

"Huyu msichana bado anakataa kuwa yeye hajaua. Najua ameua ila hawezi kukubali, kwa sababu mazingira yote yanaonyesha kuwa yeye ndiyo muuaji."

"Ni kweli Inspekta, kila kitu kinaonyesha hivyo. Hakukuwa na mtu yeyote kwenye gesti hiyo kwa wakati huo. Ulikuwa ni mchana ambapo mara nyingi huwa hakuna wateja wengi. Msichana wa zamu wa kaunta ambaye tulimkamata mwanzo, anasema hakukuwa na wateja wengine zaidi yao na hakuna mtu yoyote zaidi yao. Afande asitupotezee muda ni wakati sasa wa kuipeleka mahakamani," Koplo Hamisi alishauri.

"Sawa leo ni Ijumaa, ikifika Jumatatu asubuhi, litakuwa tayari limeshakamilika kwa ajili ya kupeleka mahakamani. Ila kwa kumsaidia, kifungu kiwe kuua bila kukusudia, sasa huko mbele kwenye ushahidi ndiyo itajulikana kama aliua kwa kukusudia au la."

"Sawa afande."

********************************

Alikuwa kama haamini kile alichokuwa akikisoma kwenye gazeti la Nipashe. "Ni Burhan huyu huyu au mwingine?" Alijiuliza.

Aliinua simu na kumpigia Koplo Hamisi. Alipoingia kwenye ofisi yake alimkabidhi gazeti na kumwambia asome pale alipokuwa anasoma yeye.




**Wakati hao watatu wakiwa hawajulikani wameuawa na nani, lakini wametupwa porini kwa pamoja, Burhan yeye anatuhumiwa kuuawa na mpenzi wake aliyekuwa naye ndani ya gesti hiyo.**

"Ni kweli. Na hili tukio tayari limeshaipotiwa hapa na jalada analo Inspekta Tausi. Ni kesi ya uporaji, lakini hali ndiyo kama ilivyo." Koplo Hamisi alijibu.

"Basi ule mpango wa kumpeleka mahakamani mtuhumiwa kwanza usimamishwe, maana kama kuna ushahidi mwingine mpya ambao tunaweza kuupata na kutusaidia kwenye kesi hii."

"Ni kweli afande." Koplo Hamisi alijibu.

Alikuwa ni Inspekta Kenneth Msiya. Alikuwa wa kwanza kufika ofisini na kupitia magazeti kadhaa. Kwenye gazeti la Nipashe lilikumbushia ile habari ya majambazi kuvamia na kupora mamilioni, kwenye gari la kusambazia pesa kwenye kituo cha kutolea pesa, maarufu kama ATM maeneo ya Mwenge jijini Dar es Salaam wiki mbili zilizopita.

Inasadikiwa zilikuwa zaidi ya shilingi milioni mia moja ambazo zilikuwa zikisambazwa kwenye vituo mbalimbali jijini Dar es Salaam.

Habari mpya zinasema kuwa, majambazi watatu waliokuwa wameshiriki kwenye tukio hilo wamekutwa wameuawa na kutupwa maeneo ya Kimara.

Inaonekana kuwa waliuawa pamoja na watu ambao hawajulikani na wala si askari polisi.

Habari zinasema kuwa kwenye tukio hilo la ujambazi waliovamia ni majambazi wanne, watatu wameuawa na watu wasiojulikana, lakini mmoja aliyebaki ametambuliwa kama Burhan Kokoto.

Hata hivyo, jambazi hilo nalo lilikutwa limeuawa kwenye gesti ya Tukutane huko Mburahati.

Wakati hao watatu wakiwa hawajulikani wameuawa na nani, lakini wametupwa porini kwa pamoja, Burhan yeye anatuhumiwa kuuawa na mpenzi wake aliyekuwa naye ndani ya gesti hiyo.

Na kwa maana hiyo, majambazi wote wanne walioshiriki uporaji huo, wote wamekufa.

Hata hivyo haijulikani pesa zilizoporwa zaidi ya milioni mia moja ziko wapi.

"Nimeanza kupata picha." Inspekta Msiya alijisemea.

Aliinua tena simu na kumtuma Koplo Hamisi amlete Mwanaidi kwenye ofisi yake.

Dakika kumi baadaye mbele yake kulikuwa na mtuhumiwa Mwanaidi na afande Hamisi.

"Endelea na kazi nitakuita."

"Sawa afande."

Alimtaza kwa makini mtuhumiwa Mwanaidi aliyekuwa amesawijika kutokana na kukaa kwa muda wa zaidi ya wiki moja sasa mahabusu.

Ni msichana mrembo na Inspekta Msiya anakiri hilo. Lakini hilo la kumuua mpenzi wake, ndilo lililomtisha afande huyo na kumuona kama pamoja na urembo wake, lakini ana kasoro.

"Nataka unisaidie kitu na mimi nitakusaidia kwenye hili tatizo." Aliacha maneno hayo yaelee hewani na kwenye kichwa cha Mwanaidi.

Hakukuwa na jibu lolote kutoka kwa Mwanaidi ambaye alikuwa haelewi, afande anataka kusema kitu gani.

"Marehemu Burhan alipokuja gesti, au mlipoongozana na kuingia gesti alikuwa amebeba nini?"

Mwanaidi aliinua uso juu na ilionekana kama anataka kukumbuka kitu.

"Ndiyo, alibeba kitu kama kiboksi hivi na alikuwa amekiweka kwenye mfuko."

"Mfuko gani?"

"Hii mifuko iliyoingia siku hizi baada ya kupigwa marufuku mifuko ya plastiki."

"Alikwambia mna nini ndani, au ulipata kuchungulia?"

"Hapana?"

"Wewe ulihisi mna nini ndani?"

"Sijui, ila alionekana hataki kabisa mimi nijue mle mna nini kwenye mfuko."

"Kwa nini ulihisi hivyo?"

"Mwanzo nilitaka kumpokea mfuko, akakataa wakati huwa nampokea sana mizigo na mifuko yake tukikutana. Halafu kila nikitaka kama kuonyesha kama nataka kujua ndani mna nini, akanikataza. Na hata tulipoingia gesti, aliuweka chini ya meza, kiasi kwamba ilinishangaza hata mimi." Mwanaidi alijibu akionyesha kuwa na uhakika na alichokisema.

Inspekta Msiya alionyesha kuwa bado na mashaka na baadhi ya majibu yake.

"Uliporudi kununua soda, uliukuta mfuko huo?"

"Afande, mimi niliporudi nilikutana na tukio la Burhan kuwa kwenye dimbwi la damu, ameuawa, sasa ningejuaje? Yaani niangalie maiti halafu, baadaye niangalie mfuko upo kweli? Ilikuwa zamu ya Mwanaidi kuuliza.

"Kwani nyinyi polisi mlipokuja na kukuta mwili wa Burhan na mimi nimezimia mfuko mliukuta?"

Inspekta Msiya alitabasamu kuulizwa swali na mtuhumiwa, lakini akaamua kujibu "Hatukukuta mfuko."

***********************

"Sasa nadhani tumepata sababu." Inspekta Msiya alimwambia Koplo Hamisi.

"Ni kwamba Burhan alikwenda kwenye gesti ya Tukutane akiwa na pesa alizoziiba na wenzake."

Na inawezekana yeye ndiye aliyewaua wale watatu ili achukue zile pesa peke yake, lakini amekutana na msichana mtoto wa mjini ambaye amemuua na kuchukua pesa."

"Afande inawezekana kabisa kuwa msichana huyu amemuua Burhan kwa sababu ya zile pesa."

"Ni kweli kwa sababu ameniambia kuwa marehemu alikuwa na mzigo ambao alikuwa nao makini hataki mtu aushike. Sasa fikiria, ameuawa kwa kisu, ndani kuna mtu, na kiasi cha pesa kama kile, unafikiri nani amechukua?"

"Lakini msichana alikuwa amezimia afande."

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# CHELSEA YATANGAZA KUPATA FAIDA




**LONDON,** England

CHELSEA imetangaza faida ya pauni milioni 32.5 katika matokeo yao ya hivi karibuni ya kifedha licha ya kushuka kwa mapato kwa sababu ya janga la virusi vya corona.

Klabu hiyo ya London ilitoa takwimu zao za hivi karibuni za mwaka ulioishia Juni 31, 2020 na ilifafanua faida iliyopatikana ingawa mauzo yalishuka kwa sababu ya COVID-19.

Mauzo yalikuwa yameanguka kutoka pauni milioni 446.7 hadi pauni milioni 407.4 kwa sababu ya virusi vya corona kama mapato ya utangazaji, siku ya mechi na mapato ya kibiashara yote yalipungua kutokana na virusi hivyo.

Chelsea walipata hasara ya pauni milioni 96.6 katika miezi 12 iliyopita, lakini kufuzu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na mauzo kadhaa ya wachezaji yalionekana kama sababu kuu za matokeo mapya.

Eden Hazard alikuwa mchezaji mkuu kuondoka Stamford Bridge wakati huo na alijiunga na Real Madrid kwa makubaliano ambayo mwisho wake yalikuwa na thamani ya karibu pauni milioni 150.

Matumizi ya Kocha wao, Frank Lampard, kwenye dirisha lililopita la uhamisho pamoja na ada kubwa kwa Timo Werner, Kai Havertz, Ben Chilwell, Hakim Ziyech na Edouard Mendy, hayakujumuishwa kwenye takwimu.

# Evans ajifunga Leicester hadi 2023

**LONDON,** England

MLINZI wa Leicester City, Jonny Evans, amesaini mkataba mpya wa miaka miwili ambao utamweka katika klabu hiyo ya Ligi Kuu England hadi mwisho wa msimu wa 2022-23.

Beki huyo wa kati wa zamani wa Manchester United mwenye umri wa miaka 32, alijiunga na Leicester kutoka West Brom Juni mwaka 2018 na amecheza mechi 89 kwenye mashindano yote.

Evans ameichezea Leicester michezo 74 ya Ligi Kuu England na amekuwa kwenye kikosi kilichoshinda mara 34, sare 15 na kupoteza 25.


Leicester inajivunia asilimia kubwa ya ushindi katika Ligi Kuu na Evans katika timu (asilimia 45.9), bila yeye (asilimia 44.4).


Leicester pia ina alama kwa wastani wa juu wa (1.6) jumla ya michezo yote wakati wakiwa na Evans kwenye timu, kuliko wakati ambao hakuwa kwenye timu (1.4).

"Nimependa hapa tangu siku ya kwanza nilipoingia. Ni mazingira mazuri na ni klabu iliyo na hamu kubwa ya mafanikio," alisema Evans akiiambia tovuti ya Leicester.

"Wachezaji wana hamu ya usajili ambao wamefanya kwa miaka mingi, wamesajili wachezaji wachanga, wenye njaa na imekuwa nzuri kwangu kuingia pamoja na hiyo na kuwa sehemu yake."

Kikosi hicho cha kocha, Brendan Rodgers kwa sasa kinashika nafasi ya tatu kwenye Ligi Kuu England, wakiwa na alama nne nyuma ya vinara Liverpool, na watacheza na Newcastle United ugenini Jumapili.




# *Barcelona kumrudisha Garcia*

**BARCELONA,** Hispania

MLINZI wa Manchester City, Eric Garcia, mwenye umri wa miaka 19, amefikia makubaliano binafsi na timu yake yake ya zamani Barcelona ili kujiungana nayo baada ya mkataba wake utakapomalizika katika majira ya joto.

Garcia alikataa kuongeza mkataba mpya City na inasemekana amekubaliana mkataba wa awali wa miaka mitano na klabu hiyo ya Katalunya.

Barcelona wanahitaji kwanza kukubaliana na City ili kukamilisha dili hilo wakati timu hiyo ilikataa dau la pauni milioni tisa katika dirisha kubwa la usajili msimu uliopita.

Kulingana na ripoti kutoka nchini Hispania, zinasema Barcelona wanahitaji kukamilisha dili la Garcia katika dirisha hili la Januari.

Lakini kama watashindwa kufikia makubaliano na City, watashuhudia mchezaji huyo akiondoka kama mchezaji huru katika dirisha la majira ya joto.

# Klopp akiri kufanya kosa uteuzi wa nahodha

**LIVERPOOL** England

KOCHA Jurgen Klopp, amekiri kufanya kosa ya kutompa unahodha, Mohamed Salah kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Katika mahojiano aliyoyafanya na kituo cha televisheni cha Diario AS, Salah alisema hakuridhishwa na kitendo cha Klopp kumnyima unahodha kwenye mchezo dhidi ya Midtjylland na alienda mbali zaidi kwa kuzungumzia uwezekano wa kutimkia Real Madrid au Barcelona.

Na Klopp ameweka wazi kuhusu kosa alilolifanya kwenye sakata hilo na amekiri kukosea kwake.

Klopp amesema alizungumza na Salah kuhusu suala hilo na alifanya kosa kumpatia unahodha Trent Alexander-Arnold katika mchezo huo uliochezwa nchini Denmark.

"Nilikuwa nahodha kwa sehemu kubwa ya maisha yangu ya uchezaji, sijawahi kuona umuhimu wake. Hakuna cha ziada unachokipata sana sana ni kuwa na kazi kubwa tu," alisema Klopp.

"Sikuwahi na sioni umuhimu wa kuwa nahodha. Kabla ya mchezo (dhidi ya Midtjylland) sikuona umuhimu wake kwa wachezaji, wala sikudhani kama ingekuwa ni habari kubwa kwa Trent.

"Hapa (Liverpool) tunasheria ya kuwa na kamati ya wachezaji. Kamati hiyo ni Jordan Henderson, James Milner, Virgil van Dijk na Gini Wijnaldum. Kimsingi hawa ndio manahodha wetu wanne.

"Kama wote hawachezi basi kawaida mchezaji aliyekaa muda mrefu kwenye timu ndiye anakuwa nahodha. Ndivyo nilivyokuwa ninaitizama, na hapo ni Trent. Simaanishi kwenye safari yake ya uchezaji chipukizi, ninazungumzia kucheza kikosi cha kwanza.



# CAVANI APIGWA NYUNDO MECHI 3




**MANCHESTER,** England

EDINSON Cavani amefungiwa michezo mitatu baada ya kupatikana na hatia ya kutumia lugha ya kibaguzi kwenye ukurasa wake wa mtandao wa kijamii.

Chama cha Soka cha England (FA), kimemfungia Cavani kufuatia chapisho alilolilweka kwenye mtandao wa Instagram, Desemba 17, mwaka jana. Chapisho hilo limetajwa kukiuka sheria na kanuni za nchi hiyo zikihusishwa na ubaguzi wa rangi.

Licha ya Cavani kukiri kuwa hakuwa na lengo baya kwa chapisho lile na kuomba msamaha kwa kueleweka vibaya sambamba na kulifuta chapisho lile, FA kwa kusimamia sheria imechukua hatua ya kumfungia michezo mitatu na kumtoza faini ya pauni 100,000.

Kwa adhabu hii, Cavani atakosekana kwenye mchezo dhidi ya Aston Villa wa jana Ijumaa, na fainali ya Carabao Cup dhidi ya Manchester City pamoja na mchezo wa mzunguko wa tatu wa Kombe la FA dhidi ya Watford.

# *United wampa mkataba Lingard*

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United imemwongezea mkataba nyota wake, Jesse Lingard kupitia kipengele kinachowaruhusu kuongeza mwaka mmoja.

Nyota huyu mwenye umri wa miaka 28, alikuwa ni sehemu ya kikosi cha England kilichofikia hatua ya nusu fainali za Kombe la Dunia mwaka 2018, na mpaka sasa ameichezea mara mbili tu United msimu huu akiwa chini ya kocha, Ole Gunnar Solskjaer.

Mkataba wa Lingard ulikuwa unamalizika kipindi kijacho cha majira ya joto, lakini United wameamua kuongeza mwaka mmoja na hivyo atasalia klabuni hapo hadi mwaka 2022.

Awali kulikuwa na uvumi kwamba, Lingard atauzwa kipindi cha dirisha dogo la usajili wa Januari hii.

Ole Gunnar amesema kuwa nyota huyo alilazimika kujitenga katika mazoezi ya peke yake mara kadhaa kwa sababu ya virusi vya corona na amesisitiza kuwa anafanya jitihada katika mazoezi.

"Anafanya jitihada kwenye mazoezi. Kwa bahati mbaya amelazimika kujitenga mara kadhaa, kwa sababu ya kupata virusi vya corona au kukaribia kupata au kuwa karibu na waathirika hata kama hakuwa nayo yeye," alisema Ole Gunnar.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MAN CITY YAJIPANGA KUMSAJILI KANE

●●● Imeelezwa wametenga dau nono kuhakikisha wanamnasa straika huyo wa Spurs...

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester City imeingia kwenye rada za kutaka kumsajili nahodha wa Tottenham Hotspur, Harry Kane, gazeti la Daily Mail limeeleza.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, Manchester City wametenga kiasi cha pauni milioni 90 kwa ajili ya nyota huyo wa Timu ya Taifa ya England.

Straika huyo anayetegemewa na Jose Mourinho, anaangaliwa na Kocha wa City, Pep Guardiola kama mrithi wa muda mrefu wa Sergio Aguero.

**Aguero hajawa kwenye kiwango cha kuvutia msimu huu, huku akisumbuliwa na majeruhi ya mara kwa mara na pia umri wake ukionekana kumtupa mkono.**

Kane hajafanikiwa kushinda taji lolote katika maisha yake ya mpira, akiwa na medali ya mshindi wa pili katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kane amecheza mechi 15 akiwa na Spurs msimu huu akifunga mabao tisa na kutoa pasi za mwisho 10, huku akiwa na kadi ya njano moja.

Manchester City wakikamilisha usajili huu itakuwa ni moja kati ya usajili bora ilizowahi kufanyika katika klabu hiyo kwa kipindi cha muda mrefu.

## ZISIKUPITE

### LINGARD, UNITED SAFI

MANCHESTER United imemwongezea mkataba wa mwaka mmoja kiungo wa kati wa England, Jesse Lingard na sasa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 atakaa klabuni hapo hadi mwaka 2022. ***(Sky Sports)***

### WIJNALDUM AJIPANGA

KIUNGO wa Uholanzi, Georginio Wijnaldum mwenye umri wa miaka 30, ameiambia Liverpool kwamba anataka kutia saini mkataba mpya, lakini pande hizo mbili bado zinatofautiana kuhusu masharti ya mkataba huo. Huku mkataba wake wa sasa ukitarajiwa kumalizika msimu ujao. ***(90 Min)***

### BOTMAN ANUKIA LIVERPOOL

LIVERPOOL imeanza mazungumzo na wakala wa Sven Botman mwenye umri wa miaka 19, ambaye anatarajia kuwasilisha ombi la kumnunua nyota huyo wa Lille na Uholanzi. ***(The Transfer Window podcast)***

### KHEDIRA ATAJWA EVERTON

KIUNGO wa kati wa Juventus na Ujerumani, Sami Khedira mwenye umri wa miaka 33, ambaye mkataba wake unakamilika mwishoni mwa msimu huu atazungumza na Everton kuhusu uhamisho. ***(Mail)***

### ARSENAL YAMSUBIRI ISCO

ARSENAL inajianda kumnunua kiungo wa kati wa Real Madrid na Hispania, Isco kwa kipindi cha msimu uliosalia, lakini wanasubiri kuona iwapo klabu hiyo ya Hispania itamwachia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28. ***(Goal.com)***

### PAPASTATHOPOULOS SAFI

MLINZI wa kati wa Arsenal na Ugiriki, Sokratis Papastathopoulos mwenye umri wa miaka 32, anakaribia kufikia makubaliano yakujiunga na klabu ya Uturuki ya Fenerbahce. ***(Takvim)***

### BARCA, GARCIA SAFI

MLINZI wa Hispania, Eric Garcia mwenye umri wa miaka 19, amefikia makubaliano binafsi na Barcelona kujiunga na atajiunga nao mara mkataba wake utakapomalizika kipindi cha majira ya joto kijacho. ***(CBS Sports)***

### ROMA, BENFICA VITANI

WINGA wa Leicester, Demarai Gray mwenye umri wa miaka 24, ambaye mkataba wake unakamilika mwisho wa msimu huu, ananyatiwa kama mchezaji huru na klabu za Roma na Benfica. ***(Sun)***

### HAALAND HAENDI BARCA

WAKALA Mino Raiola amepinga madai kwamba mshambuliaji wa Borussia Dortmund na Noway, Erling Haaland, 20, atajiunga na Barcelona iwapo Emili Rousaud atashinda uchaguzi wa urais katika klabu. ***(90 Min)***

### SIMAKAN AGOMBEWA

CHELSEA imejiunga na AC Milan na Nice katika mbio za kuwania saini ya mlinzi wa Timu ya Taifa ya Ufaransa na Strasbourg, Mohamed Simakan ambaye ana umri wa miaka 20. ***(Le10 Sport)***

HABARI MICHEZO

## Prisons yafunguka ilivyopoteza ushindi

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Prisons, Salum Mayanga, amesema Yanga isingeweza kufunga bao la kusawazisha kama wachezaji wake wasingeanza 'kupaki basi' baada ya kupata bao la mapema baada ya kipindi cha pili kuanza.

Yanga ililazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Tanzania Prisons katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Nelson Mandela Mjini Sumbawanga juzi.Mayanga alisema awali wachezaji wake walicheza vizuri kwa kuwasukuma Yanga na kuwalazimisha kurudi nyuma na hata wakishambulia si kwa nguvu kubwa kama ilivyokuwa katika kipindi cha kwanza na kabla ya kupata bao.

"Tulielekezana kuwa tucheze pasi fupi, lakini mvua ikasababisha tubadilishe mfumo. Tumeanza vizuri dakika 15 za mwanzo kwa kuhimili presha ya Yanga na tukafanikiwa, baadaye na sisi tukavuka kwao. Kipindi cha pili tulipopata bao, Yanga waliongeza presha, kitu ambacho wachezaji wangu wakaogopa na kuamua kurudi nyuma, tukawapa nafasi kutushambulia zaidi na hicho ndicho kilichotugharimu," alisema Mayanga.

Hata hivyo, Mayanga amewapongeza vijana wake kwa kupambana katika mchezo huo ambao ulimalizika kwa kugawana pointi.

"Sijaridhika na matokeo, kwenye mechi ya leo (juzi), nililenga kupata pointi tatu kwa sababu ukiangalia kwenye msimamo sisi hatuko vizuri, kwa hiyo sijafurahishwa na sare, ingawa si mbaya kwa sababu vijana wangu wamepambana dhidi ya timu kubwa na ngumu ya Yanga, sasa nakwenda kuangalia mechi inayofuata," alisema Mayanga.

## Yondani, Makame wapewa 'mikoba'

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Polisi Tanzania, Malale Hamsini, amesema ujio wa wachezaji wawili wapya, Kelvin Yondan na Abdul-Aziz Makame umeongeza ushindani katika kikosi chake kinachoshiriki Ligi Kuu Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Malale alisema wachezaji hao wanastahili kuwapo klabuni hapo na anatarajia uzoefu wao utaisaidia Polisi Tanzania.

"Maingizo mapya ya wachezaji ambao tumewasajili katika dirisha dogo ni bora, ninaimani wataleta mafanikio ndani ya kikosi chetu," alisema Malale.

Kocha huyo alisema katika mechi ya juzi wachezaji wake wameshindwa kutumia vyema nafasi walizotengeneza na hivyo wakashindwa kutimiza malengo ya kuzibakisha pointi tatu nyumbani.

"Safu yetu ya mbele imekuwa na tatizo hilo kwa kipindi kirefu kitu kinachoniumiza kichwa, lakini niweke wazi mchezo ulikuwa na ushindani, nimeumia kukosa pointi tatu nikiwa nyumbani, ila bado ninawaomba mashabiki wetu wazidi kutuunga mkono," Malale alisema.

Amewataka wachezaji wake kuongeza umakini ili wafanye vizuri katika mechi zinazofuata ambazo zitawapa mwelekeo wa msimu huu.

# USHINDI WAIPA AZAM FC MATUMAINI MAPYA

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, amesema kuanza vyema kwa timu yao kwenye mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara ni ishara njema ya mwendelezo wa kupata matokeo chanya katika michezo inayofuata ya ligi hiyo.

**Azam FC juzi iliibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya wenyeji wao, Polisi Tanzania katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Ushirika Moshi na kufikisha pointi 32.**

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam muda mfupi baada ya kurejea wakitokea Moshi jana asubuhi, Vivier alisema mechi hiyo ilikuwa ya ushindani mkubwa, lakini wachezaji wao walipambana kutafuta pointi tatu muhimu jambo ambalo walifanikiwa.

Vivier alisema anawapongeza wachezaji wao kwa kucheza kwa juhudi kwa sababu haikuwa mechi rahisi kwa pande zote mbili na ushindi walioupata unawarejesha kwenye mbio za ubingwa.

"Tulianza vizuri mzunguko wa kwanza dhidi ya Polisi Tanzania, halikadhalika na duru la pili tumeshinda na kurejea nyumbani na pointi tatu muhimu, hii ni ishara nzuri ya kuendelea kufanya vyema katika mechi zetu zijazo," alisema Vivier.

Kocha huyo alisema kwa sasa wanajiimarisha ili kusaka ushindi mechi inayofuata pamoja na kuelekea katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi yanayotarajia kufanyika visiwani Zanzibar.

"Napenda kuweka wazi kutokufanya vizuri katika mechi zilizopita, haimaanishi imetuondoa kwenye mbio za kuwania ubingwa wa ligi, bado hatujapoteza nafasi, tutapambana hadi mwisho," alisema kocha huyo.

Naye golikipa chipukizi wa timu hiyo, Wilbol Maseke ambaye amepandishwa kutoka kikosi cha U-20, ambaye juzi alidaka mechi ya kwanza ya Ligi Kuu alisema haikuwa kazi kubwa kwake kwa sababu alifuata maelekezo aliyopewa na mwalimu mazoezini.

"Bado mapema sana kujiona nimecheza vizuri sana, kwa sababu ni mechi yangu ya kwanza katika ligi na kupata matokeo mazuri baada ya kupata sare mfululizo katika mechi zetu nne za nyuma," alisema Wilbol.



Beki wa Azam FC, Nickolas Wadada (kulia), akimtoka nyota wa Polisi Tanzania, Daruwesh Saliboko, katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Chuo cha Ushirika Moshi, mkoani Kilimanjaro juzi. Azam ilishinda bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

# *Namungo yaenda Sudan ikijiamini*

**Na Saada Akida**

WAWAKILISHI wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, Namungo FC wanaondoka nchini kesho kuelekea Khartoum, Sudan kwa ajili ya mechi ya maruadiano dhidi ya El Hilal Obeid itakayochezwa Januari 5, mwaka huu jijini humo.

Katibu Mkuu wa Namungo FC, Ally Suleiman, aliliambia gazeti hili maandalizi ya safari hiyo yamekamilika na tayari walitanguliza ujumbe Khartoum kwa lengo la kuweka mambo vizuri.

Suleiman alisema kwa upande wa wachezaji, wote wako katika hali nzuri na wako tayari kwenda Sudan kukamilisha kazi waliyoianza hapa nyumbani wiki iliyopita.

"Kuna mtu (jina la kiongozi), ametangulia kwa ajili ya kuandaa mazingira ya kufikia timu yetu, usafiri wa ndani na sehemu ya kufanyia mazoezi, huyo ni mtumishi wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kwa uzoefu wake tumemwomba atusaidie hayo mambo," alisema katibu huyo.

Naye Kocha Mkuu wa Namungo, Hemed Morocco, alisema baada ya ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Coastal Union, wanarejesha nguvu kwa ajili ya mechi hiyo ya marudiano ya kimataifa.

"Tunatoka Tanga na kurejea Dar es Salaam kwa ajili ya maandalizi ya safari yetu ya Januari 3, mwaka huu kuelekea Sudan, huko tutakwenda kupambana kutafuta matokeo chanya ili tusonge mbele," Morocco alisema.

Aliongeza dhamira yao ni kusonga mbele katika michuano hiyo, hivyo watashuka dimbani kwa ajili ya kusaka mabao ya mapema na kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kupata ushindi.

# Michezo

Jumamosi Januari 2, 2021

Nipashe




City yajipanga kumsajili Kane

UKURASA 22



Golikipa wa Newcastle United, Karl Darlow (kushoto), akiwahi kuokoa shuti lililopigwa na mshambuliaji wa Liverpool, Mohamed Salah, katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa kwenye Uwanja wa St. James' Park juzi usiku. Timu hizo zilitoka suluhu. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA: MSIMU HUU HATUTAPOA

## ●●● Lakini yalia kukosa bahati Sumbawanga huku straika wake mpya akitua kibabe...

**Na Saada Akida**

WAKATI mabosi wa Yanga wakisisitiza kusajili mshambuliaji wa kiwango cha juu katika dirisha dogo lililofunguliwa, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Cedric Kaze, amesema kikosi chake hakikuwa na bahati kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Tanzania Prisons iliyochezwa kwenye Uwanja wa Nelson Mandela Mjini Sumbawanga juzi.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Kaze alisema katika kipindi cha kwanza wachezaji wake waliiga mfumo wa wapinzani wao wa kucheza mipira mirefu jambo lililoruhusu wenyeji wao kupata bao.**

Kaze alisema timu yake iliamka katika kipindi cha pili, ilicheza vizuri na ilitengeneza nafasi nyingi tofauti na ilivyokuwa kwenye dakika 45 za kwanza.

Kocha huyo alisema mbinu ambayo waliingia nayo ni kucheza pasi fupi fupi, lakini wachezaji wake walikubali kucheza aina ya mpira uliotumiwa na wapinzani wao ambao walicheza zaidi mipira mirefu.

"Tatizo lilianza pale wachezaji wangu walipokubali kufuata Prisons wanavyocheza, lakini kipindi cha pili tulibadilika na kufanya mashambulizi, ila nina imani haikuwa bahati yetu kushinda," alisema Kaze.

Naye Deus Kaseke alisema kwa kupata matokeo ya sare ni sawa na wamepoteza mechi kwa sababu mipango yao ilikuwa ni kupata pointi tatu.

Kaseke ambaye kwa sasa amekuwa kwenye kiwango bora alisema bahati haikuwa kwa Yanga na mpira ni mchezo wa makosa, hivyo anaamini kocha wao ataendelea kuyafanyia kazi upungufu kwa ajili ya kufanya vizuri katika mechi zinazofuata.

"Uwanja sio sababu kubwa ya kufanya vizuri, sema hatukuwa na bahati, pia mvua ilichangia kutopata matokeo ya ushindi, uwanja haukuwa rafiki kwa wachezaji wote," alisema Kaseke.

Aliongeza msimu huu wamejipanga kuhakikisha wanaendelea na rekodi yao ya kutopoteza mchezo wowote wa Ligi Kuu Tanzania Bara. Naye Mkurugenzi wa Uendeshaji wa Kampuni ya GSM ambao ni wadhamini wa Yanga, Hersi Said, alisema mchakato wa kumtambulisha nyota wao mpya unatarajia kukamilika hivi karibuni.

"Kila kitu kuhusu usajili wa mchezaji wetu mpya upo tayari na atakuja kuongeza nguvu kikosini, kikubwa mashabiki wasiwe na mashaka tutafanya vizuri, tumesema tuna jambo letu," Said alisema.

Hata hivyo kiongozi huyo alisema hawawezi kumweka hadharani mchezaji huyo, ili kuepuka kurudia makosa waliyofanya miaka ya nyuma ambapo walishindwa kumpata nyota waliyemtarajia.

"Haturudii makosa, siku za nyuma tuliwahi kuweka hadharani wachezaji wetu wakapata matatizo, kilichopo kwa sasa ni kuona wachezaji wanakuja nchini baada ya kukamilisha taratibu," alisema bosi huyo.

Yanga yenye pointi 44 ndio inaongoza katika msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa imecheza mechi 18 bila kupoteza hata moja ikifuatiwa na mabingwa watetezi wa ligi hiyo, Simba yenye pointi 35, lakini ikiwa na mechi tatu mkononi.

# Sven: Hesabu zitazungumza

**Na Mwandishi Wetu**

HATUTAWAANGUSHA! Hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, kuelekea mchezo wa marudiano wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya FC Platinum utakaochezwa Jumatano kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini, Dar es Salaam.

Wageni FC Platinum watashuka uwanjani wakiwa mbele kwa bao 1-0, shukrani kwa kiungo mshambuliaji wao, Perfect Chikwende ambaye alifunga katika mechi ya kwanza iliyochezwa Mjini Harare.

Sven aliliambia gazeti hili wamejiandaa kutumia vyema dakika 90 zilizobakia na jambo zuri wao watakuwa wenyeji wa mchezo huo wa marudiano.

Kocha huyo alisema kikosi chake kinaendelea na mazoezi vizuri kwa ajili ya kujiimarisha kuelekea mchezo huo ambao utakuwa mgumu kwa timu zote, licha ya wapinzani wao kuwa mbele.

"Hatukupoteza mechi hiyo ya kwanza kwa sababu tulikutana na timu nzuri, tuliadhibiwa kutokana na makosa yetu tuliyofanya. Lakini baada ya kuyafanyia kazi, nina hakika tutakuwa katika kiwango bora na tutawapa furaha mashabiki wetu," alisema kocha huyo.

Mbelgiji huyo aliongeza kucheza mbele ya mashabiki wao ni moja ya sababu inayowapa ngumu ya kuhakikisha wanasonga mbele kwenye michuano hiyo inayosimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

"Tutakuwa imara zaidi kwa sababu tunahitaji kushinda. Tumejiandaa kutorudia makosa ambayo yalitugharimu katika mchezo wa kwanza, tumejiimarisha kiufundi ili tutimize malengo yetu ya kupata ushindi mnono kwenye uwanja wa nyumbani," Sven aliongeza.

Hata hivyo, bado Sven hajaweka wazi kama nahodha na mshambuliaji kinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara, John atakuwa sehemu ya mchezo huo baada ya kuikosa mechi ya kwanza ugenini.

Simba ilifika hatua hiyo baada ya kuiondoa Plateau United ya Nigeria kwa kuwafunga bao 1-0 wakati Platinum iliichapa Costa De Sol ya Msumbiji mabao 2-1 Mjini Maputo na ilipokuwa Harare ilishinda magoli 2-0.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >